
KITENGO CHA 1

# MASHUJAA WA IMANI

SHULE YA JUMAPILI




## KITABU CHA MWALIMU

Kwa umri wowote

# MASHUJAA WA IMANI

Mtaala wa Shule ya Jumapili kutoka "Watoto ni Muhimu"
Kitabu cha Mwalimu
Kwa umri wowote
Kitengo cha 1: masomo 1-13

Tovuti:
www.ChildrenAreImportant.com/heroes/


## Shukrani Kwa Wote katika Timu ya "Watoto Ni Muhimu"!

Mhariri Mkuu: Kristina Krauss
Timu ya Ubunifu: Abril Palacios Camacho, Dwight Krauss, Jennifer Sánchez Nieto, Julio Sánchez Nieto, Mike Kangas, Monserrat Duran Díaz, Suki Kangas, Verónica Toj, na Vickie Kangas.
Shukrani kwa Rubén Dario kwa muziki wa ajabu katika programu hii.
Timu ya Watafsiri:
Ali Atuha, Aline Xavier, Annupama Wankhede, Waraka Publications, Baraka Jacob, Carla Mayumi, Chrisbresnahan, David Raju, Ephraim Njuguna Mirobi, Finny Jacob, Geenav, Jacob Kuruvilla, Krauz1, Marcos Rocha, Mathew Das, Nassim Bougtaia, Paul Mwangi, Paul Septan, Rubina Rai, Sabrina Benny John, na SubtitleMe.

# INTRODUCTION

**KARIBU...** katika Shule ya Jumapili ya Mashujaa wa Imani! Katika mfululizo huu wa mafunzo, tutaangazia orodha ya Mashujaa wa Imani inayopatikana katika Waebrania 11. Kwa sababu maisha yetu ya kiroho ni muhimu zaidi kuliko maisha yetu ya kimwili, tutajifunza jinsi tunaweza kuwa na maisha ya imani. Tutachambua ni kwa nini maamuzi ya kiroho ni muhimu zaidi kuliko maamuzi ya kawaida ya maisha. Kisha tutajibu maswali haya tunapoendelea kuchunguza maisha ya wanaume na wanawake ambao waliamini Mungu, waliongea na Mungu, na walioshi kwa ajili Yake. Wao ni kielelezo kwetu. Wakati mwingine tutaona vitendo vyema ambavyo watu walitenda na wakati mwingine tutajifunza kutokana na makosa yao.

Ingawa tunafundisha madarasa haya kwa watoto wadogo na vijana, pia wewe utapata fursa nzuri ya kujifunza mambo ya kujifurahisha kutoka kwa Agano la Kale. Zaidi ya yote, itasisimua sana kugundua njia bunifu za kutumia kanuni hizi katika maisha yetu ya kila siku. Tulifurahia sana kujifunza zaidi kuhusu Mungu na maisha ya Kikristo tulipokuwa tukiandika kitabu hiki.

Na kwa sababu tunazungumzia kuhusu Imani katika Mungu, hebu tuanze kwa kutoa ufafanuzi. Mstari tutakaotumia ni Waebrania 11:1 "Basi, imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni uhakika wa mambo tusiyoyaona. "Kuwa na imani katika Mungu ni kuamini kuwa Anaishi hata ingawa hatumuoni. Imani hiyo hutoka kwa Mungu, kwa kawaida kupitia Biblia. Na kwa imani hiyo, tunaweza Kumwamini na kuamini ahadi Zake, na kisha tufanye Yale anayotaka—kutenda kulingana na mapenzi ya Mungu.

Biblia ni kitabu cha muhimu sana kwa Wakristo wote, lakini ni kitabu kikubwa. Sio kila mtu ameweza kusoma Biblia yote. Biblia ni kubwa sana kiasi kwamba hata sisi walimu inatushinda, na tunajipata tumechanganya utaratibu wa jinsi mambo yalivyotendeka, bila kujua ni wapi na lini yalitendeka. Hebu fikiria jinsi watoto wanaiona Biblia! Ili kuelewa hili, pia tutafanya ukaguzi wa Agano la Kale na kisha kutoka kwa hadithi za Waebrania 11. Tutajifunza hili, na kisha tutajifunza jinsi kufanya Biblia iwe sehemu ya maisha yetu ya kiroho. Watoto watajifunza majina ya vitabu vya Agano la Kale na matukio mengine muhimu, yaliyowekwa katika utaratibu wa kihistoria ili wasichanganyikiwa ni lini na wapi matukio yalitendeka.

Sababu nzuri ya kujifunza Agano la Kale ni kwamba tunapata hadithi na maelekezo mazuri ambayo tunaweza kuyatumia katika maisha yetu ya sasa. Mungu ametupa Neno lake, ili tuweze kuwa mashujaa katika maisha yetu ya kila siku, huku tukimtumikia Mungu na wengine.

Kazi yako ya msingi, ikiwa utaikubali, ni kutumia masomo haya katika maisha yako ya kila siku na kuwa mfano mzuri kwa watoto na vijana, ukiwa nyumbani, darasani, na hata kanisani. Ingawa wanafunzi wako watafanikiwa kukariri mambo kutoka kwa Biblia, lengo kuu ni wao kutenda yale wanayojifunza kila wiki. Lengo lako ni kuzingatia jinsi wanavyoweza kutumia mafunzo haya katika maisha yao ya kila siku.

Tunahitaji jibu lako SASA. Taarifa hii itajifuta baada ya sekunde 10.

Mungu ayabariki maisha yako unapoendelea kuwaongoza watoto na vijana walio karibu nawe kujifundisha somo hili la "Mashujaa wa Imani".

Kwa upendo,

Timu ya ubunifu ya Watoto ni Muhimu




# JINSI YA KUTUMIA NYENZO HII

## Hadithi ya uhitaji/ suluhisho

"Mwalimu bora sio yule anawapa wanafunzi wake maarifa, lakini yule anayefanya waelewe umuhimu na wawe na hamu ya kutafuta maarifa." -MJ Berrill

Ili wanafunzi wako watumie mafundisho haya katika maisha yao, wanahitaji sio tu umakinifu darasani lakini pia motisha. Wengi hujaribu kuwapa motisha kwa kutumia pipi na zawadi au kuwaadhibu ikiwa hawana umakinifu. Ingawa mbinu hizi mbili zinawafanya wawe na tabia njema darasani, hazitoi motisha wowote kwao KUISHI kulingana na kanuni walizosoma wanaporudi nyumbani. Sisi kama walimu wa watoto katika makanisa ya Kikristo, kazi yetu sio kutumbuiza watoto ili wasiwasumbue watu wazima. Badala yake, kazi yetu ni kukuza kizazi kipya cha waumini wanaomfuata, wanaomjua na wanaomtumikia Mungu. Ingawa kazi hii ni ngumu kwa kila mmoja wetu, jambo la ajabu ni kwamba Mungu mwenyewe anajali kila mtoto zaidi kutuliko, na anatupa nguvu zake ili tuweze kuendelea na kutupa hekima yake ili tumpe motisha na kumhudumia kila mtoto.




Ili kukusaidia kuwapa motisha wanafunzi wako, tunatoa "Hadithi ya Uhitaji" mwanzoni mwa kila somo ili kuwasaidia wanafunzi WATAMBUE uhitaji wao kwa Mungu na KUTUMIA kile wanachojifunza katika maisha yao halisi ya nyumbani.Kila hadithi inajumuisha mmoja ya wahusika 5 wa uongo ambao tumeunda. Tafadhali jisikie huru kubadilisha majina yao. Wazo moja ni kuwaomba wafanyakazi wa kujitolea kuigiza hadithi kila wiki. Ikiwa hilo haliwezekani, basi unaweza kusoma tu hadithi kwa watoto kwa sauti ya juu. Unaweza kuwaomba watoto wachangie mawazo ya kutafuta suluhisho. Usiwaambie kama mawazo yao ni mabaya, mazuri, si sahihi, au ni sahihi, na usitoe suluhisho lolote bado. Tumia tatizo lililopo ili kuwafanya watoto kuwa makini zaidi na somo.

Sehemu ya Suluhisho inakuja baada ya somo. Ikiwa watoto walikuwa wameketi kwa muda mrefu, fanya shughuli kabla ya sehemu ya Suluhisho. Ukiwa tayari, wakumbushe watoto kuhusu Hadithi ya Uhitaji na kisha waigizaji wako watatokea ili kutoa suluhisho au kueleza suluhisho. Hii itasuluhisha changamoto kwenye sehemu ya hadithi ya uhitaji na kuwasaidia watoto kukabiliana na changamoto za shuleni na nyumbani.Kwa njia hii, utawapa watoto motisha wa kutumia mafundisho haya katika maisha yao ya kila siku!





WOW! YEAH!!

## Somo Kuu

Mtaala huu ni muhtasari wa jumla wa Agano la Kale. Katika masomo mengi, tutaangazia maisha yote ya mtu fulani, au Shujaa, kwenye Biblia. Kama mwalimu, unaweza kutumia maelezo haya kupata uelewa na kusoma vifungu vya Bibilia vilivyoorodheshwa kabla ya darasa ili kupata ufahamu mpya. Muhtasari wa maisha ya kila shujaa umejumuishwa katika somo kuu. Jisikie huru kuwaomba watoto wachangie maelezo zaidi ya maisha ya shujaa ili kuchochea umakinifu wao.
Tafadhali hakikisha sehemu ya hadithi ni fupi, ili kuwa na muda wa kutosha wa kueleza jambo kuu: jinsi ya kutumia. Mwishoni mwa kila somo kuna nafasi ya watoto kufanya uamuzi. Uamuzi huu ndio jambo kuu katika somo nzima, ni kama kufunga mbao kwenye mchezo wa kandanda (soka). Katika kandanda hata ukicheza vizuri, upitishe mpira kwa wenzako na uzuie timu pinzani kupata mpira, lakini hufungi mbao, basi huwezi kushinda. Hakikisha unafika kwenye jambo kuu ili kuwasaidia watoto kulitumia katika maisha yao. Katika Yakobo 1:22-24 tunasoma, "Basi muwe watendaji wa neno na wala msiwe wasikilizaji tu, ambao wanajidanganya wenyewe. Tenda kile inachosema. Kwa maana kama mtu ni msikilizaji tu wa neno na wala hatekelezi alilosikia, atafanana na mtu ajitazamaye uso wake katika kioo, na baada ya kujiona alivyo, huenda zake na mara moja husahau anavyofanana." Katika 1 Wakorintho 10, tunasoma kwamba hadithi katika Agano la Kale ni mifano inayoonyesha tunachopaswa kufanya na kile hatupaswi kufanya. Kuangazia Mashujaa wa zamani ni kama kujiangalia kwenye kioo na hutupa fursa ya kujifunza kutoka kwa maisha yao. Hebu tuwafundishe watoto kufuata mifano ya mashujaa hawa na wajifunze kutokana na makosa yao na waishi kwa ajili ya Mungu.

## Mstari wa wakati

Kila wiki watoto wanachora mstari kwenye mstari wa wakati katika vitabu vyao ili kuwakilisha maisha ya shujaa wa hadithi ya Biblia. Kwa mfano, katika somo la 1, wanapata maisha ya Adamu kwenye mstari ulio na namba 1 katika somo la 1. Kwa kutumia namba zinazotolewa katika somo, watoto wanapaswa kubaini mwanzo wa mstari na urefu wake. Kila mraba unawakilisha miaka 100. Kwa mfano, maisha ya Adamu inaanza siku ya 6 ya uumbaji na inaishia katika miaka 930, au miraba 9 na 1/3 kwenye mstari wa wakati. Itashangaza sana kugundua maisha na maelezo ya kila shujaa, kwa mfano wakati kutoka Adamu mpaka kifo cha Nuhu ni karibu sawa na wakati kutoka kwa Ibrahimu hadi Yesu kuzaliwa!




* Tarehe iliyopangwa ya ratiba ya wakati wa Biblia    * Kila mstari ni sawa na miaka 100

## Kazi

Kifaa kingine cha kuwasaidia watoto kutumia mafundisho ni kuwapa kazi ya nyumbani ya kila wiki. Kila somo lina shughuli ambayo watoto wanaweza kufanya katikati ya wiki.

Katika Yohana 14:23, Yesu alisema, "Mtu akinipenda atashika mafundisho yangu.na Baba yangu atampenda, nasi tutafanya makao yetu kwake."
Kwa kazi hizi, watoto wanaweza kutenda maishani yao kulingana na Mungu katikati ya wiki, sio tu kanisani. Kwa wanafunzi wakubwa pia kuna kazi ya kusoma Biblia. Chukua dakika chache darasani ili kujadili kazi ya nyumbani na kuwapa fursa ya kufanya mazoezi katika darasa. Toa thawabu kwa wale wanaomaliza kazi ya wiki iliyopita kwa pipi ndogo au zawadi.





## Mahudhurio / Mchezo wa mashujaa

Nyenzo hii inakuja na seti ya kadi ili kuwapa watoto watakaohudhuria kila wiki. Hizi zinaweza kuwa kadi au stika za mahudhurio. Hata hivyo, inaweza pia kuwa mchezo! Mwishoni mwa kitengo (baada ya masomo 13, au miezi 3), watoto wanaweza kutumia kadi hizi ili kucheza mchezo.Soma maagizo ya mchezo kwa maelezo zaidi.

## Mchezo mbadala

Fanya watoto waandike namba 1 hadi 10 kwenye kipande cha karatasi.Kisha mwalimu anauliza maswali yoyote kati ya 10 iliyotolewa kutoka kwa maelekezo ya mchezo. Usitaje sifa katika mabano. Kwa kila swali, wanafunzi wanaandika ubora au sifa zinazohitajika katika hali hiyo: Nguvu, Uadilifu, Utiifu, Unyenyekevu, Huruma au Imani. Atakayepata majibu mengi sahihi anashinda pipi ndogo au zawadi.

# 1. AMINI MUNGU



**Hadithi ya Biblia: Uumbaji**
**Mwanzo 1: 1-2: 3, Waebrania 11: 1-3**

## Fungu La 1 La Kumbukumbu

"Basi, imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni uhakika wa mambo tusiyoyaona." Waebrania 11:1

## Hadithi ya 1 ya Uhitaji



Katika shule ya Jumapili Buzz alifundhishwa kuhusu uumbaji, akaambiwa kwamba Mungu aliumba dunia nzima katika siku sita. Siku chache baadaye akaenda shuleni, kisha mwalimu akafika na kumwambia aangalie kitabu cha biolojia na na kuona kuwa binadamu alitoka kwa nyani. Hili likamchanganya Buzz sana. Akasema "Kanisa wananifundisha jambo moja. Shuleni wananifundisha jambo tofauti."

## Somo Kuu la 1

Karibu kwenye "Mashujaa wa Imani" mtaala mpya wa somo la shule ya Jumapili ambapo tunatoa muhtasari wa jumla wa mafundisho ya kale kwa kutumia Waebrania sura ya 11, ambapo Paulo anatupa orodha ya mashujaa wa imani.Katika somo hili la Agano la Kale, tutagundua kwamba kulikuwa na watu wengi wenye ujuzi au kazi tofauti. Kulikuwa na wakulima, mama, wachungaji, wapishi, wafalme na watumishi. Hata hivyo, tutaona kwamba katika maisha ya kila mhusika, maamuzi ya kiroho waliyofanya kila siku yalikuwa na umuhimu zaidi kuliko maisha yao ya kimwili au kazi zao. Je! Unajua utakuwa nini ukiwa mkubwa? Ungependa kuwa mzima moto, daktari, mhandisi, mchungaji, mwalimu, au fundi? Tunapowaza kuhusu maisha yetu, tunafikiria kazi zetu, au nafasi na cheo chetu katika jamii. Hata hivyo, mambo haya si muhimu kwa Mungu kama mioyo yetu na uhusiano wetu na Yeye. Mungu ana mpango maalum juu ya maisha yako!

Katika hadithi ya leo ya Biblia, tunajifunza kuhusu uumbaji, wiki ambayo Mungu alisema na ulimwengu ukawa. Biblia inasema kwamba kwa imani tunaamini kwamba ulimwengu uliumbwa kwa amri ya Mungu,  hivyo kile kinachoonekana hakikutoka kwa kile kilichokuwa. (Waebrania 11: 3) Mwanzoni Mungu aliumba dunia katika siku sita kama ilivyoelezwa katika sura ya 1 na 2 ya Mwanzo.

Siku ya 1: Usiku na mchana
Siku ya 2: Anga na bahari
Siku ya 3: Ardhi na mimea
Siku ya 4: Nyota, jua na mwezi
Siku ya 5: Wanyama wa bahari na ndege
Siku ya 6: Wanyama wa ardhi na wanadamu

Biblia inatupa utaratibu wa Mungu katika mwanzo wa dunia, na jinsi tulivyoumbwa. Mungu aliumba dunia yetu na ulimwengu katika siku 6, na aliumba Adamu na Hawa kama wanadamu wa kwanza na kuwaweka katika bustani ya Edeni.Siku ya 7, Mungu alipumzika kutoka kwa kazi Yake.

Watu wamekuwa wakiamini mambo mengi tofauti. Kama Buzz, unaweza kwenda shuleni na kuambiwa kuhusu madadiliko ya ulimwengu na jinsi dunia imekuwepo kwa mabilioni ya miaka. Wakati mwingine watu hubuni njia za kuonyesha jinsi tuliumbwa ili kuepuka kumwamini Mungu, na hutumia sayansi

kujaribu kuthibitisha njia hizi. Kama Wakristo, tunazingatia historia, na tunaamini kwamba tuna kitabu kinachoitwa Biblia, kinachotupa utaratibu wa kihistoria wa jinsi ulimwengu ulianza.
Namwamini Mungu, naamini ni Yeye aliumba ulimwengu na naamini kwamba Biblia inatoa utaratibu sahihi wa historia. Mungu ana mpango mwema juu maisha yangu, na nimechagua kumwamini.

## Suluhisho la 1



Sasa Buzz anaelewa watu wanamini mambo tofauti. Mbeleni watu waliamini dunia ilikuwa bapa, kwa mfano, lakini sasa tunaamini kitu tofauti. Leo tunajifunza kwamba Mungu aliumba ulimwengu na vitu vyote ndani yake.

## Shughuli ya 1

Unapenda nini zaidi?
Uliza kila mtoto kile anachopenda katika kila siku ya uumbaji na kile angefanya ingekuwa ni yeye.



Siku ya 1 Unapenda nini zaidi: mwanga au giza?
Siku ya 2 Ungependa kuogelea kama samaki au kupeperuka?
Siku ya 3 Unapenda nini zaidi, mchana au usiku?
Siku ya 4 Unapenda mmea au mti upi zaidi?
Siku ya 5 Unapenda ndege au samaki wagani zaidi?
Siku ya 6 Unapenda mnyama wa mamalia mgani?
Siku ya 7 Je! Huwa unafanya nini siku ya kumpumzika?

## Mstari wa 1 wa wakati

Chora mstari wa maisha ya Adamu.
Swali: Adamu alizaliwa lini? Jibu: siku ya 6 ya Uumbaji
Swali: Adamu aliishi kwa miaka mingapi? Jibu: miaka 930.

## Majibu 1 ya Mafumbo

Hapo mwanzo **Mungu** aliumba **nuru** na **akaona** ya kuwa ni **njema** na akaiita nuru, "mchana," na **giza akaliita**, "usiku."Siku ya **pili** Mungu aliumba **mbingu**. Siku ya tatu, Mungu **aliumba** nchi kavu na akusanyiko ya maji **akayaita**, "bahari" na pale **pakavu** akapaita, "nchi". Na aliumba mimea ya majani; **miche** itoayo mbegu na **miti** inayozalisha matunda.Siku ya nne aliumba **nyota** , jua na **mwezi** .Siku ya tano aliumba **wanyama** wa baharini na ndege.Siku ya **sita**, aliumba **wanyama wa mwitu** na wanyama wa kufugwa; Aliumba mwanamume na mwanamke, akawabariki na akawapa **mamlaka** ya kutawala yote aliyoumba.

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| N | D | J | S | U | K | I | 6 | T | U | M | A |
| S | I | U | 6 | I | J | A | B | M | U | U | D |
| M | O | L | N | U | K | U | A | B | A | B | N |
| B | S | I | A | I | 6 | D | 6 | I | T | I | U |
| I | M | U | L | A | A | M | U | N | O | B | P |
| H | U | M | U | N | O | T | K | G | Y | L | U |
| D | N | B | A | H | A | R | I | U | N | I | U |
| R | G | W | 6 | I | K | U | S | I | C | U | 6 |
| A | M | A | Y | N | A | W | I | Z | E | W | M |
| B | I | B | L | I | A | N | E | N | O | Y | T |



## Maswali na Majibu ya 1

1. Tungekuwa tunakaa vipi kama Mungu angetuumba kama roboti? (Hakuna mtu angeweza kunywa pombe, kuvuta sigara, nk, lakini hatungekuwa na furaha tuliyo nayo. Tungependa kuwa kama watumwa, hatungekuwa huru).
2. Unataka kumtumikia Mungu kwa njia gani siku zijazo? (Wahimize wanafunzi wajadili suala hili. Kumbuka kwamba Mungu ametoa vipaji tofauti kwa kila mmoja, na mkono wa mwili wa Kristo sio bora kuliko jicho au vinginevyo).
3. Je! Ni maamuzi gani muhimu zaidi katika maisha yetu? (Maamuzi ya kiroho, kumtii Mungu, kuamua tutakayemuoa, kumtii Mungu hata katika mambo madogo, nk).
4. Wanadamu wanatoka wapi: nyani, mlipuko au kutoka kwa Mungu? (Kuwa na majadiliano kabla ya kufikia jibu sahihi).

## Mchezo wa 1

Kijifuko cha maharagwe



Tengeneza bodi kubwa ya bango na kuandika mstari ukiwa umegawanywa katika sehemu ndogo. Katika mchezo huu, watoto watafanya mazoezi ya kukariri fungu.

• Mwalimu anaanza mchezo kwa kutupia mtoto kijifuko cha maharagwe au mpira.Mtoto anapaswa kusimama na kukariri sehemu ya kwanza ya fungu.
• Baada ya mtoto huyu kukariri sentensi anamrushia mtoto mwingine kijifuko cha maharawe ambaye anakichukua na kukariri sehemu inayofuata ya fungu hilo.
• Mtoto anaondoka mchezoni ikiwa:
  - Hasemi maneno haraka
  - Hatasimama
  - Hatasema sentensi kwa sauti ya juu (anaongea kwa upole)
  - Au anarudia maneno ya mtoto aliyetangulia
• Baada ya kila mtu kuwa na nafasi ya kukariri, mnaweza kucheza tena, wakati huu kwa kasi zaidi na kuendelea mkiongeza kasi kwa kila zamu.

## Mahudhurio ya 1




Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:

Uumbaji

## Kazi ya 1 ya nyumbani

### Kazi

Kazi yako wiki hii ni kuchukua picha ya selfi au kuchora vitu rahisi ambavyo Mungu aliumba wakati wa wiki ya uumbaji.
Jumatatu: selfi / mchoro wa mchana na wa usiku.
Jumanne: selfi / mchoro unaoonyesha anga na mwingine bahari, ziwa, au mto, ikiwa inawezekana.
Jumatano: selfi / mchoro wa mimea na miti.
Alhamisi: selfi / mchoro wa jua na mwingine wa mwezi au nyota.
Ijumaa: selfi / mchoro wa samaki na mwingine wa ndege, ikiwa inawezekana.
Jumamosi: selfi / mchoro wa wanyama na watu.
Jumapili: pumzika kutoka kwenye kazi yako ya nyumbani.

### Soma

Siku 1: Mwanzo 3:1-10
Siku ya 2: Mwanzo 3:11-19
Siku ya 3: Mwanzo 3:20- 4:2
Siku ya 4: Mwanzo 4:3-16
Siku ya 5: Mwanzo 4:17-26

# 2. MPE MOYO WAKO



**Shujaa: Habili**
**Mwanzo 4:1-16, Waebrania 11:4**

## FUNGU LA 2 LA KUMBUKUMBU

"Nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa akili zako zote na kwa nguvu zako zote." Marko 12:30

## Hadithi ya 2 ya Uhitaji



Ilikuwa mapema siku ya Jumamosi, baba ya Comet aliingia kwenye chumba chake, akamwamsha na kumwambia, "Mwanangu, tafadhali safisha gari langu.Napaswa kuondoka baadaye, na sina wakati wa kuliosha." Comet akaamka na kuanza kufanya kazi yake ya nyumbani, akasafisha ua ndogo nyuma ya chumba chake, akaondoa takataka. Alifanya kila kitu isipokuwa tu kile baba yake alimwomba afanye, kwa sababu hakutaka kufanya hivyo. Baada ya kufanya yote haya alikwenda dukani na kumnunulia babake zawadi. Baba yake aliporejea, Comet alikutana naye mlangoni na kumpa zawadi aliyokuwa amenunulia. Baba yake hakumshukuru wala kumkumbatia, kwa sababu alihuzunishwa na mwanawe kutofanya alichomwomba.

## Somo Kuu la 2

Karibu tena katika "Mashujaa wa Imani!" Jana tulijifunza kuhusu kumwamini Mungu. Tunataka kuishi kwa njia ambayo inaonyesha kwamba tunaamini Mungu. Leo tutaangazia ndugu wawili ambao wote wawili walifanya kitu cha kuonyesha imani yao kwa Mungu, lakini mmoja alimfurahisha Mungu kwa kweli na mwingine hakufurahisha Mungu.

Katika Mwanzo 4, tunapata Adamu na Hawa ambao walikuwa na wana wawili, Kaini ambaye alikuwa mkulima na Habili ambaye aliwa mchungaji. Wote wawili walitoa sadaka kwa Mungu kutoka kwa kazi zao. Kaini alitoa mazao, lakini Habili alitoa "sadaka ya wazawa wa kwanza wa kondoo wake na nyama nono." Walipoona kwamba Mungu alifurahishwa na sadaka ya Habili lakini sio sadaka ya Kaini, Kaini akakasirishwa sana na Abeli. Mungu alimuonya, lakini badala ya kumtii Mungu, Kaini alimwua Habili! Mungu aliadhibu Kaini kwa sababu ya kumwua ndugu yake kwa kumfukuza mbali na familia yake na kumpa kazi ngumu.

Wakati mwingine tunapomfuata Mungu, tunajipata tukifuata kanuni badala ya kufanya kile kinachopendeza Mungu. Kama Comet alivyofanya kwenye hadithi, sisi hujaribu kila kitu kumpendeza Mungu ila kitu moja tu, kile Yeye anataka zaidi. Tuko makini sasa kuepukana na matusi na uvutaji wa sigara, na tunazingatia sana kuhudhuria kanisa kila wiki, lakini wakati mwingine tunafanya hivyo kwa sababu tunajali kuhusu yale Wakristo wengine watasema kutuhusu. Yesu alisema ''hali ninyi mnapenda kupokea sifa kutoka kwenu ninyi wenyewe, wala hamtafuti sifa kutoka kwake yeye aliye peke yake Mungu?'' (Yohana 5:44). Kaini alipoonywa na Mungu asifanye kile alikuwa amepanga, angebadilisha tabia yake ili kumpendeza Mungu.Badala yake, Kaini alijali zaidi baraka za Mungu kwa nduguye. .Alijali zaidi kuhusu nafsi yake na maringo yake badala ya kumjali Mungu!

Katika Marko 12:30 Mungu anatumba tumpende kwa moyo wetu wote, kwa nafsi zetu zote, na kwa nguvu zetu zote (pia Kumbukumbu la Torati 6: 5, Luka 10:27). Habili alimpa Mungu moyo wake; kwa sababu alimpenda Mungu sana, akatoa kwa Mungu kile kizuri zaidi. Je, utatoa zawadi tupu kama Kaini, au kumpa Mungu moyo wako kama Habili?
Ninataka kumpa Mungu kile anataka: moyo wangu!

## Suluhisho la 2



Baada ya Comet kutambua kwamba baba yake hakusema chochote, alirudi kwenye chumba chake akiwa amehuzunika.Alikasirika kwa sababu baba yake hakumshukuru hata baada ya kile alichomfanyia.

## Shughuli ya 2

Maagizo ya Upendo
Toa nakala ya picha ya maagizo, moja kwa kila mtoto katika darasa.  Watoto wanaweza kupamba na rangi na kuzipeleka nyumbani.
Vikombe 2 vya matendo mazuri
Vikombe 2 vya utiifu
Vijiko 4 vya wakati bora pamoja
Glasi 1 ya maji kwa ajili ya wenye kiu
Kijiko 1 cha upendo
Kijiko 1 cha "chumvi ya dunia"




## Mstari wa 2 wa wakati

Chora mstari wa maisha ya Habili.
Swali: Adamu alikuwa na umri wa miaka mingapi wakati Habili alizaliwa? Jibu: Hakuna wakati halisi, lakini inadhaniwa kwamba Adamu alikuwa na umri wa miaka 50
Swali: Habili aliishi kwa miaka mingapi? Jibu: Hakuna wakati halisi, lakini inadhaniwa kwamba aliishi miaka 50.


## Majibu ya 2 ya mafumbo

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| K | W | U | E | P | O | T | M | O | Y | A |
| T | A | D | N | U | T | O | A | R | D | H |
| U | K | S | D | W | Y | P | Z | K | A | D |
| G | Z | J | I | O | B | E | L | A | H | U |
| U | I | K | Z | R | G | W | A | Z | I | G |
| D | H | A | M | B | I | U | A | I | Z | L |
| N | D | I | Z | I | T | K | T | N | J | E |
| J | R | N | I | L | I | B | A | H | A | B |
| W | A | I | D | H | A | M | D | B | B | I |

**KWELI AMA UONGO**

Weka mzunguko katika umbo hili ikiwa ni kweli na katika umbo hili ikiwa ni uongo.

1. Habili alikuwa mwana wa pili wa Adamu na Hawa.
2. Kaini alipenda kuangalia kondoo kuliko Habili.
3. Mungu alifurahia sadaka zote mbili kutoka kwa Kaini na Habili.
4. Kaini alimkasirikia ndugu yake na kumwua.
5. Mungu hakugundua kwamba Habili alikufa.



## Maswali na Majibu ya 2


1. Ni hali gani rahisi zaidi ya kumdanganya Mungu? (Jaribu kupendekeza hali tofauti, na sio tu kusema "hakuna" ingawa hilo ndilo jibu sahihi).
2. Watu wote wazuri wataenda mbinguni, sivyo? (Hapana. Kuwa "mzuri" haimanishi utaingia mbinguni. Kuokoka ndiko kutatuwezesha kuingia mbinguni).
3. Je, lazima niwe mjinga kwa ajili ya Kristo? (Kuna watu werevu na wajinga katika kazi zote ambao humfuata Kristo).

## Mchezo wa 2

Kurusha kwa lengo

Nakala ya mchoro wa mtoto kwenye bodi ya bango. Kata sehemu nyeusi kwenye mchoro ili kutengeneza mashimo ya kulengwa.


- Unda mipira ya karatasi kwa kila mtoto kwa kukunja karatasi.
- Waeleze kwamba wanapaswa kuweka mpira wao kwenye shimo lililo sehemu ya moyo.Haitahesabiwa ikiwa wataweka shimo lingine.
- Mpira ukiingia sehemu ya moyo, mtoto anapata alama 1.Mshindi ni yule atapata alama nyingi.



## mahudhurio ya 2

Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:

Habili




# Kazi ya 2 ya nyumbani

### Kazi

Kazi yako wiki hii ni kutoa kitu kutoka moyoni mwako. Biblia inasema kwamba chochote tunawafanyia wengine, tunamfanyia Yesu (Mathayo 25:40), hivyo tafuta fursa ya kumsaidia mtu au kumpa mtu kitu ambacho anahitaji. Hakikisha umepata ruhusa kutoka kwa wazazi wako. Usifanye kitu hatari. Usitoe kitu kwa nia ya kupata kitu kingine.

### Soma

Siku ya 1: Mwanzo 5:1-8
Siku ya 2: Mwanzo 5:9-16
Siku ya 3: Mwanzo 5:17-24
Siku ya 4: Mwanzo 5:25-32
Siku ya 5: Mwanzo 6:1-8

# 3. PENDEZA MUNGU



**Shujaa: Enoko**
**Mwanzo 5:21-24, Waebrania 11:5-6**

## FUNGU LA 3 LA KUMBUKUMBU

" Yesu akamjibu, Mtu akinipenda atashika mafundisho yangu na Baba yangu atampenda, nasi tutafanya makao yetu kwake. " Yohana 14:23

## Hadithi ya 3 ya Uhitaji



Kuna mtu mmoja aliyekuwa na wasiwasi kuhusu jambo fulani hivyo akaenda kwa rafiki yake Taffy ili kumwomba ushauri. Alisema, "Wazazi wangu wamekataa niende niwatembelee binamu zangu, na nataka kwenda ili nishiriki nao Neno la Mungu. Sijui kama ni sawa nikienda bila ruhusa yao. Naonelea nifanye hivyo, lakini sijui kama itampendeza Mungu. Nifanye nini? Pia nilitaka kuuliza kile nafaa kufanya kwenye mitandao ya kijamii. Niliona picha iliyosema kwamba nafaa nifanye kinachonipendeza, na mimi naona ni sawa nikienda kwa binamu zangu. "

## Somo Kuu la 3

Karibu tena katika Mashujaa wa Imani! Tumejifunza kumwamini Mungu na kumpa moyo wetu wote. Tutaangazia hili zaidi. Je! Umewahi kumpendeza mwalimu wako, baba yako au mama yako? Inahisi vizuri sana unapoambiwa na mtu kwamba ulifanya kazi nzuri, sivyo? Hisia nzuri inakua ndani yako na unatoa tabasamu kubwa kwenye uso wako. Hebu tujifunze kuhusu mtu aliyempendeza Mungu na kujifunza jinsi tunavyoweza kumpendeza Mungu, pia.

Zamani sana, miaka mingi iliyopita kulikuwa na mtu mmoja aliyeitwa Enoko. Hatuna maelezo mengi kumhusu, lakini tunajua alikuwa mzuri sana. "Enoko alitembea na Mungu; kisha akaondoka, kwa sababu Mungu alimchukua, "Mwanzo 5:24. Mungu alimpenda sana kiasi kwamba alimchukua! Si hilo ni la kipekee! Siku moja tutakutana naye mbinguni na kuwa na wakati mzuri naye. Katika Waebrania 11: 5-6 tunasoma kwamba "alikuwa mtu aliyempendeza Mungu." Je! Hebu fikiria jinsi ilivyokuwa yeye kumwona Mungu? Lazima Enoko alitabasamu kwa uwezo wake wote!

Njia ya kumpendeza Mungu ni kuamini Neno Lake na kutembea pamoja naye, kama Enoko. Waebrania 11:6 inasema, "Na pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu kwa maana kila mtu anayemjia ni lazima aamini kuwa yupo na kwamba yeye huwapa tuzo wale wanaomtafuta kwa bidii. "Tunamwamini Mungu, na tunamtafuta kwa kuamini na kutenda kulingana na neno lake, ambalo ni Biblia.

Mapema tulisikia kuhusu rafiki wa Taffy ambaye alitaka kujua cha kufanya. Biblia inasema tuwatii na tuwaheshimu wazazi wetu, kwa hivyo hicho ndicho anapaswa kufanya.

Biblia ni Neno la Mungu kwetu.  Tunaamini kwamba Biblia ni Neno la Mungu Lisilo na Hitilafu. (Haina makosa yoyote) Kwa njia hii tunaweza kusoma na kuamini kwamba kile inachosema ni ukweli. Siyo hilo tu, Biblia pia ni Neno LILILO HAI la Mungu!!

Neno litawezaje kuwa hai? Neno la Mungu liko hai na ni lenye ufanisi (Waebrania 4:12). Je! Umewahi fungua Biblia na neno la kwanza kuona kwenye ukurasa, ndilo ulilokuwa unahitaji siku hiyo? Wakristo ulimwenguni kote hujipata katika hali hiyo wakati mwingi. Yohana 1:14 inasema kwamba wakati Yesu

Kristo alikuja, ilikuwa kama Biblia ilibadilika na kuwa mtu na kutembea pamoja nasi binadamu! Tunaposoma na kuamini Biblia, ni kama tunatembea pamoja na Mungu, kama Enoko!
Nataka kumpendeza Mungu, hivyo naamini Biblia, kwamba haina makosa na ni kitabu changu cha maelekezo kwa maisha ya Kikristo.

## Suluhisho la 3

"Tazameni rafiki," anasema Taffy," Biblia inasema kwamba lazima uheshimu na uwatii wazazi wako.Pia inasema kwamba lazima utii mamlaka iliyo juu yako. Na njia bora ya kujua mapenzi ya Mungu sio kuuliza watu katika mitandao ya kijamii, bali ni kwa kusoma Biblia. Hapo ndipo huwa tunagundua kile Mungu anataka tufanye."

## shughuli ya 3


Fuata Kiongozi
Kwa shughuli hii, watoto wanatembea katika jozi. Biblia inasema kwamba Enoko alitembea na Mungu, na hii ni tofauti na kusema Mungu alitembea na Enoko. Ikiwa unataka kutembea na mtu, lazima umfuate, uende mbele yao, au ugeuke wanapogeuka. Watoto wanatembea katika jozi, mmoja anaongoza mwingine kwa dakika chache na kisha uwabadilishe ili mwenzake aongoze, Jua kwamba wakati mwingine sio rahisi kumfuata mtu, na lazima uwe macho na tayari kwa chochote.




## Mstari wa 3 wa wakati

Chora mstari wa Enoko.
Swali: Adamu alikuwa na umri wa miaka mingapi wakati Enoko alipozaliwa? Jibu: umri wa miaka 622
Swali: Enoko aliishi kwa miaka mingapi? Jibu: miaka 365.

## majibu ya 3 ya mafumbo




| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| W | I | Z | P | K | A | S | I | R | I | K | A |
| A | L | M | O | Y | O | E | I | M | P | O | K |
| A | P | O | K | O | N | E | H | O | A | A | E |
| I | E | A | E | B | M | E | T | I | L | A | A |
| N | N | H | A | I | D | E | Z | I | E | W | U |
| A | D | A | M | U | A | E | Z | L | S | A | G |
| M | E | I | D | I | H | A | H | S | U | Z | N |
| I | Z | I | A | A | L | I | I | S | H | I | U |
| M | W | L | A | I | N | U | D | U | T | N | M |
| U | A | A | W | T | M | I | L | A | E | U | E |
| N | G | A | I | L | B | I | B | Z | M | D | N |



## Maswali na majibu ya 3

1. Je, ni kweli kwamba Mungu aliandika Biblia? (Mungu hakuiandika, lakini alitoa mawazo kwa watu ambao waliiandika. Biblia iliandikwa na watu takariban 40 kwa kipindi cha zaidi ya miaka 1500).
2. Je, Ni kwa nini mimi si mkamilifu? (Ongea kuhusu vile Mungu alitaka tufurahie maisha, hivyo hakutuumba kama roboti. Wanadamu wote hufanya makosa, lakini Mungu husaidia yeyote anayemfuata. Pia jadili kuhusu kujithamini, upendo na neema ya Mungu).
3. Tunawezaje kumpendeza Mungu? (Kumpa mioyo yetu, kumtii, na kutumia muda wetu pamoja Naye).

## mchezo wa 3



Mbio ya Kupokezana na Torati
Katika karatasi tano, andika mojawapo ya vitabu vitano vya kwanza vya Biblia na mchoro wa mwendo unaoelezwa hapo chini.
Katika karatasi nyingine andika "Torati." Weka riboni ama kiti kwenye mstari wa kuanzia na uweke karatasi ya "Torati" kama lengo.
Weka karatasi zile tano zilizo na vitabu vya Biblia katika maeneo mbalimbali, mbali inavyowezekana na kulingana na nafasi ulionayo.
Mwendo

- Mwanzo: Nyoosha miguu na mikono.
- Kutoka: Chuchumaa.
- Mambo ya Walawi: Ruka.
- Hesabu: Pekecha.
- Kumbukumbu la Sheria: Tembea kwa mguu mmoja.

Cheza

- Tengeneza timu 2 za kushindana mbio za kupokezana.

- Kila timu inatoa mwanafunzi mmoja atakayetumia muda sawa na wengine.
- Baada ya kufikia kila karatasi, mwanafunzi anasema kwa sauti jina la kitabu cha Biblia na anaanza kufanya mwendo ulioonyeshwa, anarudia kwa kila silabi za neno.
- Baada ya kukamaliza vitabu vyote vya Torati, mwanafunzi anakimbia na kugusa lengo, na mwanafunzi wa timu nyingine anaanza.
- Wanatimu wanapaswa kukimbilia vitabu ambazo wanatimu wenzao hawajafaulu kufikia hadi sasa.
- Timu ya kwanza kufikia vitabu vyote vitano na kugusa lengo inashinda.

Rudia mchezo hadi watoto wote waweze kujifunza vitabu vyote vitano vya kwanza vya Biblia.

## mahudhurio ya 3




Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:

Torati

## Kazi ya 3 ya nyumbani

### Kazi

Kazi yako wiki hii ni kusoma hadithi kadhaa katika Agano Jipya na kushudia Yesu akitembea nawe. Andika kuhusu hali ambazo unadhani Yesu alikusaidia au kusaidia wengine kwa sababu ulimwomba kufanya hivyo. Wakati mwingine anatupa mawazo, pia, andika mawazo ambayo unadhani Yesu alikupa. Chunguza pamoja na mwalimu wako ili kuhakikisha mawazo uliyoandika yanakubaliana na Biblia.

### Soma

Siku ya 1: Mwanzo 6:9-22
Siku ya 2: Mwanzo 7:1-12
Siku ya 3: Mwanzo 7:13-24
Siku ya 4: Mwanzo 8:1-12
Siku ya 5: Mwanzo 8:13-22

# 4. KUMTII MUNGU



**Shujaa: Nuhu**
**Mwanzo 6:9-9:17, Waebrania 11:7**

## FUNGU LA 4 LA KUMBUKUMBU

"Basi muwe watendaji wa neno na wala msiwe wasikilizaji tu, ambao wanajidanganya wenyewe." Yakobo 1:22

## Hadithi ya 4 ya Uhitaji



Wazazi wa Kip walienda safari, hivyo Kip aliendа kukaa na binamu yake.Kabla ya kuondoka, baba yake alimwomba asitoke nje usiku, kwa sababu ni hatari kufanya hivyo. Wazazi wake hawakutaka kuwa na wasiwasi kwamba Kip alikuwa nje usiku. "Ni sawa baba, sitatoka nje," Kip aliwaambia. Baada ya wazazi wake kuondoka, usiku huo huo, binamu zake walimwalika kwenda mjini pamoja nao. Alivutiwa sana na wazo hilo, hivyo akaanza kubadilisha nguo zake ili kwenda nao. "Sawa, hebu tuendeni," kila mtu alisema.

## Somo Kuu la 4

Je! Umewahi sema kitu kama, "Mimi siogopi buibui" lakini ulipokutana na buibui moja ukaogopa na kutoroka? Au umewahi muahidi mama au baba yako kwamba hutafanya kile alikuonya, kisha ukamuasi? Wiki iliyopita tulijifunza kuhusu kuamini Neno la Mungu, lakini ni rahisi sana kusema tu bila kuzingatia katika matendo! Yakobo 2:26 inasema kwamba imani pasipo matendo imekufa. Leo tutajifunza kuhusu mtu ambaye imani yake ilikuwa hai sana.

Biblia inatuambia kwamba kuna wakati Mungu aliamua kuleta mafuriko duniani yote kwa sababu watu wote walikuwa waovu. Mungu akamshauri Nuhu, mtu wa pekee mwenye haki duniani, kujenga safina (boti kubwa sana).

Inaweza kuwa ngumu kumtii Mungu kwa sababu tofauti. Wakati mwingine hatutaki. Biblia haituambii kuhusu mawazo ya Nuhu, lakini nadhani yeye hakuwa mtengenezaji wa safina hapo mbeleni na ilimbidi abadilishe na kumtii Mungu.

Wakati mwingine ni vigumu kutii kwa sababu hatuelewi. Ilichukua takriban miaka 100 kujenga safina, na Nuhu alikuwa tu anaona mbingu iliyo wazi bila ishara yoyote ya mafuriko! Mtoto mdogo anaweza kosa kuelewa hatari ya barabara yenye magari mengi, lakini anapaswa kuwatii wazazi wake na kukaa mbali. Je! Wazazi wako wamewahi kukuonya usifanye jambo ambalo hukuelewa?

Wakati mwingine ni vigumu kutii kwa sababu tunajali kile wengine watasema. Hebu fikiria kile watu walisema kuhusu Nuhu. Lakini kama watu wangefikiria jinsi mambo yatakuwa siku za baadaye, wangesaidia Nuhu na kumwomba nafasi kwenye safina!

Wakati mwingine tunadhani haiwezekani. Mungu alimwambia Nuhu aweke jozi ya kila mnyama kwenye safina. Paka hazipendi maji na vitu vinavosonga kama boti na huwa hazitilii maanani! Lakini Nuhu hakupaswa kuweka tu paka, pia simba na kondoo na wanyama wote pamoja!

Noa aliitii na akajenga safina. Kisha wanyama wakamtii Mungu pia na wakajileta wao wenyewe! Dunia nzima ilifurika kwa mwaka na siku 10, na kila kitu kikaangamia! Biblia inasema kuwa anayeshika amri anasalimisha maisha yake (Methali 19:16). Kwa utiifu wa Nuhu, aliokolewa, pamoja na familia yake na

wanyama tofauti. Ikiwa unamtii Mungu, inaweza kuokoa wengine pia. Mapema tulisikia kuhusu mvulana aitwaye Kip. Alipokuwa karibu kutoka nje na binamu zake, alikumbuka yale wazazi wake walisema na kuwaambia binamu zake kwamba hakutaka kwenda nje.
Mungu aliahidi kamwe hataleta mafuriko duniani kwa ishara ya upinde wa mvua. Kila wakati unaona upinde wa mvua, fikiria kuhusu ahadi ya Mungu na jinsi unavyoweza kumtii Mungu kama Nuhu.
Nimeamua kumtii Mungu kwa sababu ni kwa manufaa yangu.

## Suluhisho la 4



Lakini kabla ya kuondoka, Kip alikumbuka maneno ya baba yake, akamwambia binamu zake kwamba hakutaka kwenda.Kip aliamua kutii wazazi wake.

## Shughuli ya 4

Nuhu Anasema




Hebu tufanye shughuli inayoitwa "Nuhu anasema" ambayo inahitaji watoto kutii "Nuhu".(Inafanana na mchezo wa kawaida wa "Simoni anasema") Nuhu anasimama mbele ya washiriki, kisha anatoa amri ya kufanya vitendo tofauti. Ikiwa Nuhu atasema, "Nuhu anasema, 'Ruka juu'," watoto wanapaswa kufanya hivyo. Ikiwa anasema "Ruka juu" bila kwanza kusema "Nuhu anasema", watoto hawapaswi kufanya chochote. Mchezaji akifeli kuzingatia amri ya Nuhu au anafanya kitendo bila kwanza kusikia "Nuhu anasema", anaondolewa mchezoni. Mchezo unamalizika ikiwa ni mtoto mmoja tu amebaki au watoto wote wakiondolewa.

## Mstari wa 4 wa wakati

Chora mstari wa maisha ya Nuhu.
Swali: Je, ni miaka ngapi ilipita tangu kuzaliwa kwa Enoko hadi kuzaliwa kwa Nuhu? Jibu: miaka 434
Swali: Nuhu aliishi kwa miaka mingapi? Jibu: miaka 950.

## Majibu ya 4 ya mafumbo

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| F | W | M | U | N | G | I | B | M | A | H | D |
| O | A | K | I | M | I | H | S | E | H | A | H |
| K | N | M | I | F | A | S | N | Y | S | I | W |
| I | Y | U | I | I | N | I | M | A | I | L | A |
| R | A | N | H | L | L | S | N | M | R | M | A |
| U | M | I | D | U | I | I | Y | A | M | A | I |
| F | A | L | K | S | F | A | S | H | A | F | N |
| A | U | V | M | A | W | E | D | N | I | P | U |
| M | A | F | S | A | H | A | D | I | L | U | D |
| I | M | U | N | G | U | M | V | U | A | R | A |





## maswali na Majibu ya 4

1. Kwa wazazi wangu huniambia cha kufanya kila wakati? (Kwa sababu wanakupenda sana na wanakutakia mema. Pia jadili ukweli kwamba wazazi ni wanadamu pia na wakati mwingine wao hukosea).
2. Je, itakuwaje kama kumuasi Mungu kutanilitea umaarufu na kuwapendeza wengine? (Jadili hali tofauti zinazohusiana na hili. Wasaidie wanafunzi kuelewa kuwa kutatokea hali ambazo watastahili kuamua ikiwa wanataka kumtii Mungu au kuwapendeza wengine).
3. Je, nitaishi nimefurahia maisha yangu yote? (Jadili kuhusu hadithi za utoto, kufurahishwa na mambo ya ulimwengu, maisha ya duniani yasiyo na tatizo, na furaha ya uzima wa milele).


## mchezo wa 4

Mfalme na malkia wanaomba!



- Chagua watoto wawili watakaoigiza kama mfalme na malkia.
- Wataketi kwenye viti vyao vya kifalme mbele ya watoto wengine.
- Baada yao kuwa tayari, mwalimu anamwuliza malkia, "Ungetaka nini?"
- Malkia anaomba kitu ndani ya chumba, na watoto wote wanakikimbilia ili kukileta, wasichana wanamletea malkia, na wavulana wanamletea mfalme.
- Kisha mwalimu anamwuliza mfalme kile anataka, na wanafunzi wanakimbilia na kumletea mfalme au malkia wao.
- Endelea mchezo kwa wakati uliopangwa.
- Timu inayotumia muda mchache, inayotii amri zaidi, na kuwa na heshima, nk, inashinda.

## mahudhurio ya 4




Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:
Nuhu

## kazi ya 4 ya nyumbani

### Kazi

Kazi yako wiki hii ni kuandika kuhusu hali moja au zaidi ambazo ulijaribiwa kufanya kitu ambacho Mungu hapendi, lakini ukaamua kufuata Mungu.

### Soma

Siku 1: Mwanzo 15:1-6
Siku ya 2: Mwanzo 15:7-21
Siku ya 3: Mwanzo 21:1-6
Siku ya 4: Mwanzo 22:1-10
Siku ya 5: Mwanzo 22:11-19

# 5. PITA MTIHANI



**Shujaa: Abrahamu**
**Mwanzo 12:1-7, 15:1-6, 21:1-3, 22:1-19, Waebrania 11:8-19**

## Fungu la 5 la Kumbukumbu

"Amebarikiwa mtu ambaye anavumilia majaribu, kwa sababu akisha stahimili atapewa taji ya uzima ambayo Mungu amewaahidi wale wampendao." Yakobo 1:12

## Hadithi ya 5 ya Uhitaji



Ulikuwa mtihani muhimu sana. Kila mtu alipaswa kujitayarisha ipasavyo kwa mtihani huu, kwa sababu matokeo yake yangetumika kuchagua wakaohudhuria Olimpiki ya ujuzi.Hivyo Peppy alitumia siku yote akisoma bila kwenda nje kucheza - alitaka kuchukua nafasi ya kwanza. Siku ikafika. Kila mtu alikuwa tayari, katika kiti chake na penseli yake. Mwalimu akafika na kutoa mtihani. Lakini Peppy alishtuka kuona kuwa mtihani ulikuwa kuhusu suala tofauti na lile alisomea.

## Somo Kuu la 5

Hebu tujifunze kuhusu mtu anayerejelewa kama baba wa imani yetu. Siku moja Mungu alimwambia Abrahamu aondoke mji wa baba yake na amfuate, na Ibrahimu akatii. Ibrahimu na mkewe hawakuwa na uwezo wa kupata watoto. Wakati ukatokea ambapo Mungu alimuahidi kuwa atampa mtoto hata ingawa alikuwa mzee sana. Na sio tu mtoto, kizazi chake kingekuwa taifa kubwa na ulimwengu wote ungebarikiwa kupitia kwake! Ibrahimu alimwamini Mungu naye Mungu akaita hii haki.

Miaka baadaye, Ibrahimu na Sara wakapata mvulana aitwaye Isaka. Miaka kadhaa baadaye, Mungu alimwomba Ibrahimu kutoa mwanawe kama dhabihu, kijana aliyemthamini sana na ambaye alikuwa ahadi ya Mungu iliyotimizwa kwa Ibrahimu! Mungu alikuwa na nia ya kumwokoa Isaka, lakini hakumuarifu Ibrahimu. Mungu alingoja kuthibitisha ikiwa Ibrahimu alimpenda.

Wakati mwingine Mungu ana mipango mikubwa juu ya maisha yetu, lakini kabla ya kutimia kwa mipango hii tunapitia mtihani. Mungu anataka kujua tunampenda kwa kiasi gani. Mungu anataka ufanye nini leo? Wakati mwingine unahitajika kuachana na jambo mbaya kama vile tabia potovu, rafiki mjeuri, kusema uongo au kuiba, au kubadilika na kuanza kumsaidia mama yako na kazi ya nyumbani. Wakati mwingine tunapaswa kuachana na mambo ambayo haionekani kuwa mabaya. Isaka hakuwa kijana mbaya. Wakati mwingine ni jambo zuri ambalo linashindana na upendo wako kwa Mungu. Kwa watu wengine, Mungu anataka waachane na masomo ya chuo kikuu kwa sababu wanachotaka tu ni cheo cha juu, na kwa wengine anataka waendelee na chuo kikuu wakati hawataki. Inaweza kuwa chombo cha muziki, mtu anayekuvutia (mtu unayependa), au kipindi unachopenda zaidi cha katuni.Wakristo wengi hawataki kuachana na kitu fulani, na hivyo wanakwama katika safari yao ya imani na kukua, kama Peppy ambaye alisoma suala tofauti kwa ajili ya mtihani. Itakapofika wakati wa kuchagua Mungu au kitu kingine, utachagua nini?

Ibrahimu alichagua kumtii Mungu katika jambo hili ngumu sana. Alimchukua Isaka hadi kilele cha mlima, akamfunga, na kumweka kwenye madhabahu. Na Ibrahimu alipokuwa karibu kumkata Isaka kwa kisu, Mungu akamzuia! Mungu alimwonyesha kondoo aliyekuwa amekwama kwenye kichaka cha karibu na akatoa kondoo huyo badala yake. Lakini ilikuwa wazi kwamba Abrahamu alimpenda Mungu zaidi kuliko chochote kingine duniani.

Mungu alifanya kitu sawa alipomtuma mwanawe wa pekee Yesu afe kwa ajili yetu. Yesu alisema kwamba chochote ambacho ungependa watu wakutendee, na wewe watendee vivyo hivyo. (Mathayo 7:12) kisha yeye akatenda kulingana na maneno yake kwa kutoa uhai wake.Mungu alitupa kila kitu alichokuwa nacho, naye anatuomba tufanye hivyo Kwake.

Nampenda Mungu zaidi kuliko kitu kingine chochote duniani kote, na nimechagua kutoa chochote anachoomba kutoka kwangu.

## Suluhisho la 5




Alikuwa na wasiwasi mwingi alipokuwa akijibu mtihani.Baada ya kila kumaliza, mwalimu alisahihisha mitihani na kutoa alama. Kila mtu alipita mtihani isipokuwa Peppy. Wanafunzi walipogundua hilo walimcheka sana. Peppy alihuzunika sana.

## Shughuli ya 5

Mtihani wa ghafla

Shughuli hii itakuwa ya kugundua kile wanafunzi wanapenda zaidi, mambo ya kidunia au ya kiroho.Waarifu watoto kwamba kutakuwa na mitihani miwili ya ghafla wakati wa darasa; bila kuwaarifu wakati sahihi.



MITIHANI:

1. Acha sarafu darasani katika sehemu inayoonekana na inayoweza kufikiwa na watoto. Wakati wa darasani, angalia uone ikiwa kuna mtoto ataziona au kile atafanya akiziona. Mtoto anapita mtihani ikiwa hatachukua sarafu.
2. Leta peremende kwa kila mtoto, lakini hakikisha kuwa peremende ni za ukubwa tofauti. Zingine ziwe kubwa na za kuvutia. Waambie wanafunzi kuwa kuna peremende kwa kila mtu na kwamba wanafaa kwenda mbele na kuchukua, mmoja baada ya mwingine. Mtoto anapita mtihani ikiwa hatachukua peremende inayovutia zaidi.
3. Wape fursa ya kutumikia. Waulize wasaidie katika kusafisha darasa baada ya somo. Mtoto atakayesafisha vizuri zaidi anapita mtihani.

KUMALIZIA: Baada ya mitihani yote mitatu, waarifu watoto aina za mitihani walizopitia, wale walipita na kueleza sababu za kupita.


## Mstari wa 5 wa wakati

Chora mstari wa maisha ya Ibrahimu.

Swali: Nuhu alikuwa na umri wa miaka mingapi wakati Abrahamu alizaliwa? Jibu: umri wa miaka 890

Swali: Abrahamu aliishi kwa miaka mingapi? Jibu: miaka 175.

## Majibu ya 5 ya mafumbo




| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | W | A | K | W | A | L | I | P | O | J | A | R |
| I | B | R | E | I | H | A | M | U | H | I | M | U |
| B | I | W | A | K | R | I | S | T | O | N | I | H |
| I | E | M | C | B | H | O | R | I | K | A | D | I |
| H | D | T | S | H | R | D | H | A | B | M | I | B |
| A | W | I | B | I | R | A | J | O | P | I | L | A |
| B | T | H | H | J | M | U | H | I | S | O | W | H |
| S | I | A | K | A | A | G | N | A | H | C | M | D |
| M | U | N | G | U | H | T | K | J | M | U | N | G |
| M | A | I | S | H | A | O | M | C | H | U | G | U |



## Maswali na majibu ya 5

1. Utafanya nini mtu mwingine akichukua nafasi yako au achukue kitu bora kwa sababu amekushinda katika jambo fulani? (Jadili jinsi unavyoweza kumwomba Mungu ili usiwe na uchungu, lakini wamsamehe mtu au mwalimu huyo. Pia jadili jinsi mtu anavyoweza kujifunza au kutia bidii ili kufanya vyema katika nafasi inayofuata).
2. Je, unakumbuka mtihani wako wa mwisho kutoka kwa Mungu? (Iwe ni watoto wadogo au wakubwa, huenda wote wamepitia hali fulani ambayo wanahisi kuwa ni Mungu aliwasaidia au kuwapa changamoto. Wape fursa ya kushiriki hali moja. Mfano mmoja katika maisha ya Kristina, mwandishi wa mtaala huu: Nakumbuka mitihani midogo nilipokuwa mdogo. Wakati mmoja niliahidi Mungu kwamba sitaenda kwenye densi yoyote. Nilidhani itakuwa rahisi sana kufanya hili, lakini kanisa langu likaandaa densi! Ikanichanganya! Ilikuwa vigumu kuweka ahadi yangu na kukosa kwenda kwenye tukio la Kanisa).

WOW! YEAH!!

3. Tunawezaje kuwa na alama za juu katika maisha yetu ya kiroho? (Katika swali hili tunapaswa kuwa makini ili tusiwafunze watoto kuwa kama Wafarisayo, na kufanya mambo kwa sababu ni ya "kidini" ili watu wengine waone.Wasaidia kugundua tofauti kati ya kufanya mambo ya kidini na kufuata Yesu kutoka moyoni. Je, kuna kitu unafanya kwa sababu unataka tu kuwapendeza wengine? Au unafanya kwa sababu unataka kumpendeza Mungu, hata kama hakuna mtu mwingine anaona? )


## Mchezo wa 5



Kisia ni nini

- Kusanya vitu kadhaa (maua, kalamu, vifungo, mpira, uta, nk).Usiwaonyeshe watoto.
- Wafunge watoto macho kwa kitambaa na kuwapa nafasi ya kukisia baada ya kunusa au kugusa nk., kitu fulani.
- Unaweza kuunda vikundi kadhaa na kuweka vitu katika mfuko na uzipitishe kwa kila kikundi, na kuruhusu watoto kugusa vitu na kukisia vitu vingi iwezekanavyo.

## Mahudhurio ya 5




Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:
Ibrahimu

## Kazi ya 5 ya nyumbani


### Kazi

Kazi yako wiki hii ni kuandikia kuhusu ndoto zako, mambo ambayo ungetaka kutimiza katika maisha yako. Usiogope kuwa na ndoto kubwa. Unaweza kuwa unataka mambo makuu, kama kuwa mtaalam wa anga, mwogeleaji, mwanajeshi, daktari, mmiliki wa biashara.Kuwa na ndoto kubwa-Mungu wako ni mkubwa. Kisha uliza Mungu ikiwa kuna kitu unachopaswa kuacha kwa ajili Yake, chunguza pamoja na mwalimu wako kuhusu hilo, kisha utekeleze wiki hii.

### Soma

Siku ya 1: Mwanzo 25:19-26
Siku ya 2: Mwanzo 25:27-34
Siku ya 3: Mwanzo 27:1-17
Siku ya 4: Mwanzo 27:18-29
Siku ya 5: Mwanzo 27:30-45

# 6. THAMINI MAMBO YA KIROHO



**Shujaa: Isaka**
**Mwanzo 25:19-34, 27:1-40, Waebrania 11:20**

## Fungu la 6 la Kumbukumbu

"Mtu atafaidi nini kama atapata ulimwengu wote lakini akayaangamiza maisha yake?" Marko 8:36

## Hadithi ya 6 ya Uhitaji



Ilikuwa mapema sana wakati mama alimwomba Buzz aende kwa nyanyake ili aombe sukari.Buzz aliamka na akaenda nyumbani kwa nyanyake. Kitu cha kwanza kuona kilikuwa sarafu. Akaitana: "Nyanya, nyanya uko wapi," hakuna yeyote alijibu. Buzz akawaza, hakuna mtu ananiona, na nikichukua sarafu hio hakuna mtu atakayenikemea kwa hivyo naweza enda na ninunue peremende. Nitaichukua, na hakuna mtu atagundua. Baada ya dakika chache, nyanyake akafika na kumpa kikombe cha sukari.

## Somo Kuu la 6

Wiki iliyopita tulijifunza kuhusu kupita mtihani. Leo tutafunza kuthamini mambo ya kiroho kuliko mambo ya kimwili.

Mwana wa Ibrahimu, Isaka, aliendelea na kukua na hata akapata familia yake mwenyewe. Badala ya kujichagulia mke, alimruhusu babake kumchagulia (Mwanzo 24). Kisha Isaka na mkewe Rebeka wakapata mapacha, Esau na Yakobo.

Siku moja Esau alirudi nyumbani kutoka mawindoni akiwa na njaa sana kiasi kwamba alidhani angekufa! Alitaka tu kitu chochote angekula na alikuwa tayari kutoa chochote kwa ajili yake! Je, umewahi kuwa katika hali ambayo ulitaka kitu fulani kiasi kwamba ungeweza kufanya kitu chochote ili ukipate? Yakobo aliamua kumhadaa Esau. Alimwahidi Esau chakula ikiwa tu atabadilishana na urithi wake, na Esau alikubali! Esau alibadilisha mwelekeo wote wa maisha yake kwa bakuli moja ya supu!!

Katika siku hizo baba angewabariki wana wake kabla ya kufariki. Isaka alizeeka sana na kupoteza uwezo wa kuona. Ikafika wakati ambapo alipanga kumbariki Esau. Lakini Yakobo alifuata ushauri wa mama yake, akavaa kama Esau na hivyo kumdanganya babake! Hivyo akachukua baraka za Esau kutoka kwa babake. Esau alidhani bakuli la supu haikuwa ya maana sana, lakini wakati alitaka kuchukua urithi wake tena, hakufaulu! Akaupoteza milele!

Isaka alithamini mambo ya kiroho. Aliamini ahadi ya Mungu kuwa kizazi chake kingerithi dunia, na akambariki Yakobo kwa ahadi hizo.

Mungu anamiliki urithi, mpango na baraka kwa kila mmoja wetu. Lakini tusipokuwa waangalifu, tunaweza kwenda kinyume na mpango huo kutokana na chaguzi zetu! Njia moja ya kufanya hivi ni kutenda dhambi. Unapodanganya na kusema ulipata alama za juu kuliko ulivyopata, utaonekana mwerevu kwa muda, lakini utakuwa umepoteza uadilifu wako! Mapema, Buzz alipanga kuchukua sarafu za nyanyake, lakini Peppy aliingia nyumbani na kumsaidia!Alimwambia kwamba nafsi yake ni ya thamani zaidi kuliko sarafu, na hivyo Buzz akaachana na sarafu.

Unapoendelea kuwa mkubwa, hatari inaongezeka. Wakristo wengi huchagua wapenzi kulingana na mwonekano au fedha badala ya kuzingatia kilicho ndani yao. Kisha, wanapotaka kumtumikia Mungu,

mwenzi wao anakuwa kizingiti. Na uamuzi wa unayemuoa ni wa kudumu! Esau alioa wanawake ambao waliwasumbua Isaka na Rebeka (Mwanzo 27:46). Kwa upande mwingine, Isaka na baadaye mwanawe Yakobo walithamini mambo ya kiroho hata walipokuwa wakichagua mke.
Yesu alisema kuwa mahangaiko ya maisha haya na anasa za mali husonga maisha yetu na kutufanya tusizae matunda na kupokea urithi wetu. (Mathayo 13:22). Hakikisha hutadharau urithi wako na kuubadilisha na kitu kingine chochote, hata ikiwa hitaji lako ni la aina gani.
Nimechagua kuthamini mambo ya kiroho ya maisha kuliko vitu vya kimwili.

## Suluhisho la 6

Wakati huo, Peppy aliingia nyumbani na kumsaidia! Akamwabia Buzz, nafsi yako ina thamani zaidi kuliko sarafu! Buzz aligundua kile alichokuwa karibu kufanya, na akarudisha ile sarafu haraka, na akamshukuru rafiki yake Peppy.

## Shughuli ya 6


Hedaya za Uamuzi
Katika shughuli hii, watoto watafunga kipande cha riboni kwenye pini ya usalama na kutumia ili kukumbuka maamuzi muhimu ambayo watafanya wiki hiyo. Riboni inaweza kuunganishwa na nguo isiyovaliwa wakati wote. Ombeni pamoja kwamba Bwana atawasaidia wafanye chaguzi za kiroho.


## Mstari wa 6 wa wakati

Chora mstari wa maisha ya Isaka.
Swali: Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka mingapi wakati Isaka alizaliwa? Jibu: umri wa miaka 100
Swali: Isaka aliishi kwa miaka mingapi? Jibu: miaka 180.

## Majibu ya 6 ya mafumbo

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S | L | R | V | T | F | S | E | M | E | S | S |
| A | E | A | I | A | N | X | S | N | N | U | N |
| D | I | T | I | D | Z | Y | A | K | O | B | O |
| B | I | L | U | N | B | N | U | E | I | I | L |
| I | A | G | I | I | I | F | G | W | S | R | A |
| M | U | R | G | W | C | T | A | Q | A | I | K |
| L | K | B | A | U | M | A | H | A | R | B | A |
| R | E | B | E | K | A | I | C | C | R | Y | P |
| B | I | B | L | I | A | A | K | A | S | I | A |
| U | P | O | F | U | O | H | O | R | I | K | B |






## Maswali na majibu ya 6

1. Ni sifa gani zinayoonyesha kwamba tunathamini ulimwengu wa kiroho kuliko ulimwengu wa kimwili? (Ruhusu wanafunzi wajadili mambo tofauti: marafiki, kazi, umaarufu, kutumikia kanisani, nk).
2. Itakuwaje ikiwa hupendi kilicho sahihi? (Ruhusu wanafunzi kueleza hali walizopitia).
3. Itakuwaje ikiwa wengine wanafanya na ni mimi pekee ambaye sifanyi? (Waruhusu wazungumzie ugumu wa kufanya jambo sahihi wakati wengine wote wanafanya kinyume.Zumngumizia hali za kipekee).

## Mchezo wa 6


Kizuri na kibaya



Ni vigumu kwa watoto kutambua kati ya kizuri na kibaya.Katika mchezo huu, tutafanya mazoezi kutambua kitu kinachowakilisha thamani ya kiroho.

Jaza vyombo viwili hadi nusu na mchele mbichi, weka pini 15 za usalama katika kila chombo. (Hakikisha pini zote zimefungwa vizuri.) Changanya vizuri mchele na pini za usalama. Tengeneza timu mbili. Funga macho ya mtoto mmoja kutoka kila timu kwa kitambaa. Mwalimu atakaposema, "Anza," watoto wote wawili waliofunikwa macho watajaribu kutafuta pini za usalama kwa mikono yao, bila kuangalia, na kupata nyingi iwezekanavyo. Wao watagundua kwamba ni vigumu sana kuskia tofauti ya mchele na pini wakitumia mikono yao. Chukua dakika chache kisha hesabu pini ambazo kila mtoto amepata. Timu yenye pini nyingi za usalama inashinda.

## Mahudhurio ya 6




Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:
Isaka

## Kazi ya 6 ya nyumbani

### Kazi

Kazi yako wiki hii ni kuandika kuhusu urithi wako, mambo uliyo na uwezo wa kufikia.Kwanza, usidhani kwamba urithi kutoka kwa familia si wa muhimu.Una maana sana. Inaweza kuwa mekanika au mhandisi, au muuguzi. Unaweza kuleta mabadiliko kwenye mtaa wako au nchi nzima.Lakini andika kuhusu urithi wako wa kiroho.Wewe ni mtoto wa Mungu na wewe ni sehemu ya familia yake kubwa. Mungu amekubariki na ujuzi na matamanio mbalimbali, na anaweza kuyatumia ili kukuwezesha kufanikiwa katika familia yake ya kiroho. Unaweza kumwonyesha walimu wako hili, lakini si lazima. Moyo wako ni wa thamani sana kwa Mungu.

### Soma

Siku ya 1: Mwanzo 28:10-15
Siku ya 2: Mwanzo 28:16-22
Siku ya 3: Mwanzo 32:1-8
Siku ya 4: Mwanzo 32:22-27
Siku ya 5: Mwanzo 32:28-32

# 7. BARAKA YA MUNGU



**Shujaa: Yakobo**
**Mwanzo 27:41-28:2, 28:10-15, 28:20-22, 31:3-13, 31:22-24, 32:9-12, 32:22-30, 33:1-11 , 35:1-5, Waebrania 11:21**

## Fungu la 7 la Kumbukumbu

" Yesu akajibu, Wamebarikiwa zaidi wale wanaolisikia neno la Mungu na kulifuata." Luka 11:28

## Hadithi ya 7 ya Uhitaji



Comet alikuwa na rafiki aliyemwalika kwenye sherehe kila wakati, lakini siku moja akagundua kwamba watoto wote kwenye sherehe walikuwa wapotovu.Hakuhisi ametosheka katika sherehe hizi. Alijua kwamba Mungu hapendi watoto wanaotenda mabaya. Kisha wakati wa likizo, rafiki yake akamwalika tena kwa sherehe na kumwambia kuwa itakuwa ya kuvutia kuliko zote. Comet alitaka sana kwenda, lakini alikuwa dhabiti na akasema, "Hapana." Rafiki yake aliposikia hili, akamjibu: "Kama huenda na mimi, usiwahi niongelesha tena. Utaachwa na rafiki ule mpoa." Hilo lilimtia Comet wasiwasi. Hakujua la kufanya. Alijua kwamba ilikuwa vibaya kwenda kwenye sherehe, lakini hakutaka kupoteza rafiki yake.

## Somo Kuu la 7

Katika maisha tunachaguzi mbili, kupigania vitu vya dunia (kimwili) au baraka za Mungu (kiroho). Baada ya kuchukua urithi wa Esau, Yakobo alitoroka kwa sababu alidhani Esau atamwua (kimwili), lakini pia alikuwa akitafuta baraka za Mungu kwa kuwatii wazazi wake (kiroho). Njiani, Biblia inasema kwamba alichokuwa nacho tu kilikuwa mkongojo (kimwili). Alipokuwa amelala, alipata ndoto ambapo aliwaona malaika wakiteremka na kupanda ngazi iliyofikia mbinguni, na Mungu akamwahidi (kiroho) kwamba atakuwa na kizazi kirefu ambacho kingemiliki dunia. Yakobo alimwomba Mungu awe pamoja naye (kiroho), kitu ambacho ni cha thamani kuliko milki yoyote.

Yakobo alikutana na jamaa yake, akaoa, akapata watoto, na kumfanyia kazi mjomba wake Labani kwa miaka 21! Mjomba wake alimhadaa mara kwa mara (kimwili). Lakini Mungu alikuwa pamoja na Yakobo na kumbariki (kiroho) na familia kubwa na mali nyingi (kimwili). Hata Labani akabarikiwa kwa sababu ya Yakobo! (Mwanzo 30:27) Wakati mwingine baraka za Mungu katika maisha yetu hufikia watu walio karibu nasi, pia. Lakini Yakobo alipokasirika na kutoroka kutoka kwa Labani (kimwili), Mungu alizungumza na Labani na kumlinda Yakobo (kiroho).

Yakobo aliogopa kurudi nyumbani! Ingekuwaje kama Esau bado alitaka kumwua? Basi akagawanya familia yake na mali yake katika vikundi ili kama kundi moja libgevamiwa, lingine lingeweza kuponea (kimwili). Wakati wa usiku, alipigana na Mungu ili ambariki (kiroho).

Lakini Yakobo alishangaa, kwa sababu Esau alimkimbilia na kumkumbatia! Naye Yakobo akampa Esau zawadi kubwa. Tunapothamini baraka za Mungu zaidi ya baraka za kimwili, tunaweza kuwa wakarimu badala ya kuogopa watu wengine.

Baadaye, Mungu alimwambia Yakobo na familia yake watupilie mbali miungu mingine yoyote, kwa hivyo wakazika sanamu zao na pete za dhahabu (kimwili). Walipofanya hivyo, mtu yeyote aliyekuwa na nia ya

kuwadhuru akaingiwa na woga! (kiroho) Yakobo alisema, "Mungu ... amekuwa nami popote nilipokwenda." (Mwanzo 35: 3)

Kama Yakobo, tunaishi katika ulimwengu wenye upande wa kimwili na upande wa kiroho. Dunia nzima inapigania mali zaidi, vichezeo, mwonekano mzuri, umaarufu, na ujuzi zaidi. Hata kuna Wakristo ambao huenda kanisani na kudai kuwa wanafuata Biblia, kisha wanatumia maisha yao wakipigania vitu vya kimwili, ingawa Yesu alisema kuwa huwezi kumtumikia Mungu na fedha (Luka 16:13).

Ni bora kupigania baraka za kiroho za Mungu. Tunaweza pigania uwepo wa Mungu, kumtumikia, kuhudumu kanisani, na kueneza injili kwa wengine. Tunaweza kupigania kufungua mioyo yetu kabisa kwa Mungu na kutoficha chochote kutoka kwake. Tunaweza pigania kuweka maslahi ya wengine mbele ya yetu na kufanya kile kinachopendeza Mungu. Yesu alisema kuwa wale wanaolisikia neno la Mungu na kulitii wamebarikiwa (Luka 11:28).Sawa na maisha ya Yakobo, wakati mwingine baraka za Mungu huja kwa mfano wa vitu vya kimwili; mara nyingi huja kama kitu kingine, kama ulinzi au moyo uliobadilika. Comet, katika hadithi ya leo, anaweza kupigania baraka za Mungu kwa kukataa kwenda kwenye sherehe.

Nimechagua kupigania baraka za kiroho badala ya baraka za kimwili.


## Suluhisho la 7



Alihuzunika sana, hivyo Taffy alipofika na kumwuliza, "Nini kibaya?" Comet alielezea kilichotokea. Lakini Taffy akamwambia kwamba hafai kuhisi vibaya - kumpendeza Mungu ndilo chaguo bora zaidi. Mungu ana marafiki wengi kuliko mtu yeyote. Usijali eti umempoteza rafiki kwa kutohudhuria sherehe. Akamsalimia na kuondoka. Comet akaelewa na kuamua kumpendeza Mungu na kutoenda kwenye sherehe hizo.

## Shughuli ya 7

Kupigania baraka



Andika "KUPIGANIA BARAKA," kwenye ubao wa bango na kuweka kwenye ukuta.Andika baraka tofauti kwenye vipande vidogo vya karatasi. Ficha karatasi za baraka chini ya vitu tofauti. Watoto wanapaswa kuzitafuta na kuzinatisha kwenye sehemu iliyoandikwa "KUPIGANIA BARAKA." Baada ya kumaliza mchezo, watoto wanasimama mbele ya ubao wa bango na kuchukua zamu kusoma baraka kwa sauti ya juu. Himiza watoto wainue mikono ikiwa wamepokea baraka yoyote waliyoisoma.

## Mstari wa 7 wa wakati


Chora mstari wa maisha ya Yakobo.

Swali: Isaka alikuwa na umri wa miaka mingapi wakati Yakobo alizaliwa? Jibu: umri wa miaka 60

Swali: Yakobo aliishi kwa miaka mingapi? Jibu: miaka 147.

## Majibu ya 7 ya mafumbo

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| D | A | L | I | Y | B | A | R | U | G | N | U | M |
| I | N | D | U | G | U | R | Y | A | K | O | B | A |
| N | A | G | A | N | A | O | N | D | O | T | O | L |
| A | W | I | K | I | R | A | B | E | Y | I | L | A |
| B | M | W | A | A | G | R | L | O | M | S | H | I |
| A | U | N | D | I | N | K | A | G | K | R | A | K |
| L | N | W | P | L | B | A | U | H | M | A | W | A |
| N | G | I | B | E | T | H | A | K | E | E | Y | E |
| I | L | E | H | T | E | B | S | N | D | L | U | G |
| A | U | M | A | L | A | I | E | K | I | I | I | U |





## Maswali na majibu ya 7

1. Je, ni makosa unapojitakia mambo mazuri? (Jaribu kuzungumzia hili. Ilikuwa vyema kwa Yakobo kupigana na Mungu ili kupata mambo mazuri. Tunahitaji kujali wengine kwanza, hata hivyo, tunapaswa kutunza nafsi na roho yetu vizuri, tukijitakia baraka nzuri juu ya maisha yetu!).
2. Cha muhimu ni kila mtu anipende, sivyo?(Waache wajadili kuhusu mvutano kati ya kupenda jirani yako lakini unamweka Mungu mbele.Biblia inasema kwamba tunapaswa kuishi kwa amani pamoja na wengine (Warumi 12:18), lakini tunapaswa tumfuate Mungu bila kujali maamuzi ya watu wengine (Yohana 21:22).Jadili hali za kipekee).
3. Naweza kupoteza baraka za Mungu kwa sababu nimekosea au kufanya kitu kibaya? (Je, unambuka somo la wiki iliyopita? Esau alipoteza kila kitu kwa sababu maadili yake yalikuwa mabaya. Yakobo alipokea baraka zaidi kwa sababu alizipigania!).

## Mchezo wa 7



Vita vya Chupa

Weka kiasi kidogo cha mchanga kwenye chupa tupu ya soda ili kuipa uzito kidogo.

- Chagua eneo la kuanza.
- Chagua mtafutaji, mtoto atakayewatafuta wengine.
- Mtafutaji atatupa chupa kwa umbali iwezekanavyo.
- Watoto wengine wanakimbia ili kujificha, wanakimbia kinyume na upande wa chupa.Wanapaswa kujificha kabla ya mtatafutaji kufikia chupa.
- Baada ya kurejesha chupa kwenye eneo la kuanza, mtafutaji anaanza kutafuta watoto waliojificha ili kuwashika.
- Akipata mmoja, wanakimbia pamoja hadi eneo la kuanza.Mtafutaji anachukua chupa na kusema, kwa mfano, "1, 2, 3, Lucy nyuma ya mti." Kisha mtafutaji anarudi kutafuta mtu mwingine.
- Yeyote ambaye bado hajashikwa anaweza kuwanusuru wengine ifuatavyo: bila kushikwa na mtafutaji, anapaswa kukimbia hadi eneo la kuanza kisha achukue ile chupa na kuitupa, na kusema, "1, 2, 3 kwa ajili yangu na marafiki zangu wote."Mtafutaji anapoteza mateka na hivyo watoto wengine wanakimbia na kujificha tena.
- Ikiwa hakuna uokoaji, na mtafutaji afaulu kuwapata wachezaji wengine wote, anashinda.
- Ili kucheza tena, mtoto aliyeshikwa wa kwanza anakuwa mtafutaji mpya.

## mahudhurio ya 7




Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:
Yakobo

## kazi ya 7 ya nyumbani

### Kazi

Kazi yako wiki hii ni kukumbuka yale uliyowaza na kuandika wiki mbili zilizopita; ndoto yako na urithi wako.Waza kuhusu mambo haya, lakini pia fikiria jinsi unaweza kuyaharibu kwa kufanya mambo fulani. Ikiwa unaasi nyumbani, inaweza kuathiri sana urithi wako wa familia .Ikiwa ndoto yako ni kuwa daktari au mhandisi, unaweza kuiharibu kwa kukosa kufanya vyema shuleni. Ikiwa ndoto yako inahitaji afya nzuri, unaweza kuiharibu kwa kuvuta sigara, kutumia madawa ya kulevya, au pombe. Andika jinsi ya kuishi ili uweze kufikia ndoto zako na urithi wako.

### Soma

Siku ya 1: Mwanzo 37:1-11
Siku ya 2: Mwanzo 37:12-24
Siku ya 3: Mwanzo 37:25-36
Siku ya 4: Mwanzo 41:1-13
Siku ya 5: Mwanzo 41:25-41

# 8. KUMTUMAINIA MUNGU



**Shujaa: Yosefu**
**Mwanzo 37:2-11, 37:17-36, 39:1-41:13, 41:14-16, 41:28-40, 41:56-42: 5, 45:1-15, 47:5 , Waebrania 11:22**

## Fungu la 8 la Kumbukumbu

" Basi, tusi choke kutenda mema, kwa sababu kama hatukuchoka tutavuna kwa wakati wake." Wagalatia 6: 9

## Hadithi ya 8 ya Uhitaji



Peppy yuko shuleni na ameketi karibu na rafiki yake Zip.Wanapenda kwenda shuleni. Asubuhi hii mwalimu aliwapa zoezi la kuandika hadithi. Peppy anapenda kuandika, hivyo akaandika na kumaliza haraka sana. Alikuwa wa kwanza kumaliza na mara moja akasema, "Mwalimu, nimemaliza" Unadhani nini kilifanyika? Mwalimu alipuuza na hakujibu. Dakika kumi baadaye Zip alimaliza na kusema, "Mwalimu, nimemaliza." Mwalimu mara moja akaja na kusema, "Zip, hadithi yako inavutia sana kusoma." Peppy alikasirika sana, akasema, "Kwa kuwa mwalimu hashughuliki na mimi, sitakuwa nafanya mazoezi yake. Huwa haangalii ninachofanya."

## Somo Kuu la 8

Jacob, ambaye tulijifunza kumhusu wiki iliyopita, alikuwa na wana 12. Mwana aliyependa sana alikuwa Joseph, naye akampa koti la kupendeza.Wakati huo huo, Yusufu akaota ndoto kwamba angetawala ndugu zake. Ndugu zake waliosikia kuhusu ndoto hili walimchukia sana kiasi kwamba walipanga kumwua! Badala yake, walimuuza katika utumwa. Mara nyingi Wakristo hudhani kwamba baraka za Mungu zitawalinda kutokana na mambo mabaya. Lakini Mungu hutumia nyakati ngumu ili kutuandaa kulingana na mpango Wake, na tunapaswa kumtumainia atafanya hivyo.

Yusufu aliuzwa kwa Potifa, mkuu wa walinzi huko Misri. Badala ya kukata tamaa, alimtumainia Mungu na alifanya kazi yake vizuri na hivyo akachaguliwa kama msimamizi wa nyumba yote ya Potifa! Mke wa Potifari alimpenda Yosefu na alitaka kulala naye. Yusufu alimwogopa Mungu na hakutaka kufanya mabaya. Ikiwa mtu atajaribu kukushawishi ufanye maovu, fanya kile Joseph alifanya: kataa hata kukaa chumba kimoja na mtu huyo. Ingawa Joseph hakuwa na hatia yoyote, alishtakiwa bila ushahidi, na akafungwa gerezani bila haki!

Yusufu alimtegemea Mungu, na Mungu akambariki kiasi kwamba akapata umaarufu gerezani lote! Muokaji na mtunza vinywaji walimkosea Farao na hivyo wakafungwa jela, na usiku mmoja wakaota ndoto. Yusufu aliamini kuwa Mungu angempa tafsiri ya ndoto zao. Muokaji alinyongwa, na mtunza vinywaji alirudishwa kwenye nafasi yake, sawa na tafsirir ya Yusufu. Lakini mtunza vinywaji akamsahau Yosefu! Haki ikakosekana tena!

Miaka miwili baadaye, Farao akaota ndoto tatatinishi, na mtunza vinywaji akakumbuka Yosefu. Yusufu alikuwa amejifundisha kumtumaini Mungu, na akaamini Mungu atamsaidia mbele ya Farao. Tafsiri ilikuwa kwamba kutakuwa na nafaka nyingi kwa miaka 7, kisha njaa kwa miaka 7. Kisha Farao akamfanya

Yusufu kuwa waziri mkuu wa Misri baada ya miaka 13 ya utumwa na kufungwa gerezani! Mungu alikuwa amemfundisha Yusufu kusimamia nchi vizuri, sio kwa manufaa yake bali kwa kila mtu.
Njaa ilikuwa mbaya kiasi kwamba kila watu wengi walifikiwa na janga hilo, hata familia ya Yusufu. Ndugu zake ambao walimuuza Yusufu kwa utumwa walihitaji Yosefu kuwasaidia na nafaka! Lakini hawakumtambua, na akawajaribu kuona kama wamebadilika. Kisha Yusufu akawasamehe na akawagawia sehemu nzuri ya nchi. Tunapomwamini Mungu, tunaweza kuwasamehe wengine na kuwafanyia wema.
Kama Yusufu, Yesu hakufanyiwa haki. Alishtakiwa kwa mashtaka ya uongo ingawa hakufanya vibaya. Kisha Yesu alisulubiwa msalabani! Kama Yusufu, alimwamini Baba yake Mungu katika changamoto hizi. Yusufu alifanywa waziri mkuu, lakini Yesu alifanywa mfalme wa ulimwengu wote! Mungu anatuomba tumtumaini katika nyakati ngumu naye anatuahidi kuwa atatembea nasi hadi mwisho. Maandiko yanasema kwamba katika mambo yote Mungu hutenda kazi pamoja na wote wampendao, wale ambao wameitwa kufuatana na mapenzi yake (Warumi 8:28).Je! Utamruhusu Mungu kutumia nyakati ngumu ili kukuandaa kwa chochote alichokupangia?
Naamua kumtegemea Mungu kwa maisha yangu, hata wakati mambo yanapokuwa magumu.


## Suluhisho la 8

Kisha rafiki yake Buzz akagundua kilichomfanyikia Peppy.Alizungumza naye na kumshawishi kuwa utiifu ni sifa ambayo kila Mkristo anapaswa kuwa nayo kila siku. Labda mwalimu hakumsikia na ndiyo sababu hakumjibu wakati alipomaliza kazi yake. Peppy alitambua kuwa tabia yake haikuwa sahihi, na aliendelea kufanya kazi vizuri pamoja na mwalimu wake.



## Shughuli ya 8

Shajara ya Ujasiri
Watoto wanatengeza shajara ya jinsi ya kumwamini Mungu wiki hii.Toa robo mbili za karatasi kwa kila mtoto. Watoto wanaweka pamoja vipande, vilivyokunjwa na kushikanishwa ili kutengeneza kijitabu. Kisha wanapamba jalada. Wanaandika katika shajara jinsi wanavyoweza kumtumaini Mungu kila siku wiki hii. Wasaidia kuandika siku ya kwanza.




## Mstari wa 8 wa wakati

Chora mstari wa maisha ya Yusufu.
Swali: Yakobo alikuwa na umri wa miaka mingapi wakati Yosefu alizaliwa?Jibu: Hakuna wakati halisi, lakini hudhaniwa kwamba Yakobo alikuwa na umri wa miaka 100
Swali: Yusufu aliishi kwa miaka mingapi? Jibu: miaka 110.

## Majibu ya 8 ya mafumbo

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| R | A | N | B | I | O | T | O | N | D |
| N | A | W | Z | U | A | W | J | A | U |
| N | D | U | G | U | R | A | A | W | G |
| K | F | O | G | N | A | P | M | M | Y |
| A | K | O | T | O | F | E | F | U | R |
| M | A | C | H | O | I | W | S | T | A |
| Z | N | M | F | R | S | U | H | M | N |
| U | Z | W | S | J | F | G | I | T | G |
| J | U | I | K | U | H | C | M | U | I |
| F | M | W | A | N | A | A | O | M | W |






## Maswali na majibu ya 8


1. Je, Kuna mambo ambayo Mungu anaweza shindwa kufanya? (Hapana, Biblia inasema kwamba Mungu ana nguvu zote. Anaweza kuona kila kitu na kuelewa kila kitu tangu mwanzo wa wakati hadi leo na milele).

2. Kwa nini Mungu huruhusu mambo mabaya kutufanyikia? (Katika hali ya Yusufu, Mungu alitumia mambo magumu ili kumwezesha kufikia mahali ambapo Mungu alitaka na pia kumfundisha.Mungu anajali zaidi mioyo yetu, hivyo vitu vingi "vibaya" sio vibaya kwetu, bali ni za manufaa kwetu. Pia ni vizuri kutambua kwamba tunaishi katika ulimwengu uliojaa dhambi, na Mungu amemruhusu shetani kufanya maovu duniani. Hivyo kuna kifo, vita, mitetemeko ya ardhi, majanga, na watu wengi wanaofanya mambo mabaya, na hayo yote huathiri Wakristo wote na wasioamini).

3. Kwa nini dini nyingine si nzuri? (Biblia inasema kuwa njia pekee ya wokovu ni kupitia Yesu Kristo. Je! Dini zingine zinasema unahitaji kufanya nini ili uwe na haki mbele za Mungu?)

# Mchezo wa 8


Mchezo wa Kamba




- Funga kamba kwenye miti au nguzo tatu tofauti zilizo angalau mita moja kwa umbali, na weka lebo zinazoonyesha nambari 1, 2 na 3.
- Tafuta wakimbiaji sita (kulingana na idadi ya wanafunzi katika darasa lako) ambao watatumika kushika watoto wengine.
- Nao watoto wengine watajipanga kwa umbo la tao takriban mita 10 kutoka kwa miti.Weka wakimbiaji sita kati ya watoto na miti.
- Mwalimu anaposema, "Shika kamba," watoto wote wanapaswa kushika mojawapo ya kamba bila kuguswa na wakimbiaji.Mtoto akiguswa anasimama palepale.
- Ikiwa mtoto anafikia kamba, na tayari kuna mtoto mwingine ambaye tayari ameshika kamba, anapaswa kushika mkono wa mtoto huyo ili kuanza au kupanua safu.Watoto wote ambao wameshika kamba au wanaunganishwa na watoto kutoka kwenye kamba hawawezi kuguswa.
- Wakati watoto wote wameunganishwa au kusimamishwa, puliza filimbi ili kuendelea na mchezo.Mwalimu atasema kamba 2 au kamba 3, na watoto ambao wameunganishwa na kamba hizo wanapaswa kuziachilia na kukimbilia kamba nyingine tofauti bila kuguswa. Watoto waliokuwa wameguswa hapo kabla pia wanaweza kukimbia wakati huo. Wakimbiaji sita watahitaji kurudi hatua sita nyuma kabla ya kuanza tena kukimbiza watoto.
- Mwalimu hapaswi kusema kamba 1 kwa sababu wakati watoto wote wako kwenye kamba 1 au wamesimamishwa basi mchezo unaisha.
- Endelea kucheza mpaka watoto wagundue kwamba wakiwa kwa kamba 1 hawatahitaji kusonga, na wote wakimbilie hapo.
- Uliza watoto sababu ya kukimbilia kamba 1, wakati kamba 2 na 3 ni tupu.
- Ongea jinsi ilivyo sawa na kumwamini Mungu.Yeye ni mwaminifu daima, na ikiwa tutamkimbilia kwanza, hatutahitaji kukimbia tena.

# mahudhurio ya 8

Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:
Yusufu




# kazi ya 8 ya nyumbani

## Kazi

Kazi yako wiki hii ni kuwasamehe watu. Sisi sote tumepitia hali ambayo tulitendewa visivyo. Tunaweza kasirika kuhusu hilo na kulipiza kisasi, au tunaweza kuchagua kusameheana na kumtumaini Mungu. Wiki hii unapowaza jinsi mtu fulani alikuumiza, waza pia, "Nimemsamehe." Si lazima umwambie, lakini unaweza lisema kwa sauti hata kama uko peke yako. Hiyo inakuachilia kutoka kwa hasira uliyonayo, na utaweza kufurahia tena.Pia utakuwa kama Baba yako wa mbinguni, Mungu, ambaye hutusamehe dhambi sisi sote. Unavyowasemehe watu wengi, ndivyo utahisi huru zaidi.

## Soma

Siku ya 1: Kutoka 3:2-10
Siku ya 2: Kutoka 7:10-11, 20-21, 8:6-8, 16-22
Siku ya 3: Kutoka 9:2-3, 6-19, 10:3-5, 21-23
Siku ya 4: Kutoka 11:4, 12:12-14, 29-30
Siku ya 5: Kutoka 14:5-9, 13, 21-27

# 9. ACHANA NA DHAMBI



**Shujaa: Musa**
**Kutoka 1:1-2:15, 3:1-12, 4:10-17, (7:8-13:42), 14:5-31, Matendo 7:20-34, Waebrania 11:23-29**

## Fungu la 9 la Kumbukumbu

"Kama mtu akijitakasa na kujitenga na visivyo vya heshima atakuwa chombo cha kutumika kwa shughuli za kifahari; chombo kilichotakaswa kimfaacho Bwana wa nyumba, ambacho ni tayari kwa matumizi yote yaliyo mema." 2 Timotheo 2:21

## Hadithi ya 9 ya Uhitaji



Comet alikuwa anakimbia dukani kwa kasi kwa sababu mamake alikuwa tayari anatengeneza chakula cha jioni na alihitaji yai mara moja.Alifika dukani na kuitana kwa sauti kubwa, lakini hakuna mtu alijibu. Kisha akagundua kulikuwa na pesa kwenye dirishani. Inaonekana, kuna mtu alikuwa amesahau pesa zake hapo. Kwa kuwa hakuna mtu aliyekuwa karibu, aliangalia zile pesa, kisha akazichukua.

## Somo Kuu la 9

Familia ya Yakobo ilipanuka na kuwa taifa la Israeli. Lakini Wamisri wakawahadaa na kuwafanya watumwa na Farao akaamua kuua watoto wao wote wachanga wa kiume. Mama mmoja Mwisraeli aliweka kijana wake kwenye kikapu na kumweka katika mto wa Nile.Bintiye Farao akamchukua na akamwita Musa. Musa alionyesha imani kwa Mungu kwa kuacha nafasi yake katika familia ya kifalme ya Misri na badala yake kuwa sehemu ya watu wa Mungu. Alitaka kuokoa Israeli, lakini dhambi yake ikamzuia. Siku moja Musa aliua Mmisri kwa kumpiga Mwisraeli. Lakini moyo wa Musa ulikuwa na dhambi nyingine: kiburi. Musa alidhani angeweza kuwaokoa Waisraeli kwa njia aliyoitaka. Biblia inasema kwamba Mungu hupinga wenye kiburi lakini huwapa wanyenyekevu neema. Mungu alitaka kufanya kazi katika moyo wa Musa jinsi tu alivyofanya kazi katika moyo wa Yusufu. Musa alipatikana na hatia na alitoroka ili kuokoa maisha yake na akaenda kuishi jangwani.

Miaka 40 baadaye, Mungu alikuja na kuzungumza naye kutoka kichaka kilichowaka moto lakini hakikuwa kinachomeka. Mungu alimwambia Musa arudi, lakini wakati huu ni Mungu angekuwa akiwaokoa Waisraeli, na Musa angefanya mambo kulingana na Mungu. Musa alitambua kwamba hangeweza kuokoa Waisraeli, kwamba hakujua kuzungumza vizuri na hakuwa na ujuzi wa kuongoza watu. Lakini hayo hayakuwa kizuizi! Mara nyingi Mungu hututumia katika mambo ambayo hatuna uzoefu, hivyo ni dhahiri kwamba Mungu anafanya kitu ndani mwetu.

Mapema leo tulisoma kuhusu jinsi Comet aliiba fedha kutoka dukani. Mungu hawezi kumtumia Comet kama yeye ni mwizi. Ikiwa tutatubu au kuachana na kiburi na dhambi zetu, Mungu ataweza kututumia. Na wakati Mungu atataka tufanye jambo, hatutaogopa kwa sababu tunajua kwamba Mungu anafanya kazi ndani yetu.

Katika Misri, Mungu alitumia Musa kuwaokoa Waisraeli na kuonyesha ukuu wa nguvu za Zake kuwahi kushuhudiwa. Mungu alileta mapigo 10 katika Misri: akageuza maji kuwa damu, vyura, viroboto, nzi, vifo vya mifugo, majipu, mvua ya mawe, nzige, giza, na mwisho kuuawa kwa wazaliwa wa kwanza wa

Wamisri Katika pigo la mwisho, Mungu aliwaamuru Waisraeli kuchinja kondoo kwa ajili ya chakula na kupaka damu yake kwenye milango ya nyumba zao. Kila nyumba iliyomtii Mungu, wana wa kwanza waliokolewa. Ilikuwa mfano wa Mungu kumtuma mwanawe Yesu afe kwa ajili yetu kama mwana-kondoo. Watu wengi hujaribu kujiokoa wakitumia njia yao badala ya kumwamini, kutubu, na kumtii Mungu. Je, utachagua njia ya Mungu?
Israeli walimfuata Mungu hadi Bahari ya Shamu, nao Wamisri walikuwa nyuma yao wakiwafukuza! Musa aliwaambia Waisraeli kwamba hawakuhitaji kuhofia, kwamba Mungu angewapigania na kuwaokoa. Kisha Mungu akagawanya Bahari ya Shamu nao Waisraeli wakavuka kwenye ardhi kavu na kuta za maji kila upande, lakini Wamisri walizama. Musa aliwaongoza Waisraeli katika maisha yake yote kwa unyenyekevu na utiifu kwa Mungu.
Naamua kutubu dhambi zangu na kukaa msafi mbele za Mungu.

## Suluhisho la 9



Comet alikuwa na fursa ya kufanya tendo nzuri na kurudisha pesa. Aliendelea kufikiria kuhusu jambo hilo, na kisha rafiki yake Peppy, aliye na uadilifu mwingi, akafika. "Nilikuwa nakuhitaji sana," Comet alisema. Kwa ushauri wa rafiki yake, alifanya jambo lililofaa na akarudisha pesa.

## Shughuli ya 9

Eleza hadithi
Kuja na magazeti au kata picha za watu, maeneo, na vitu na kuleta darasani (epuka picha zenye mauti au zisizofaa). Tengeneza timu 2 au zaidi za watoto. Kila timu inatumia picha zilizokatwa kutoka kwenye magazeti ili kuunda hadithi inayojumuisha dhambi, toba, na maisha mapya.



## Mstari wa 9 wa wakati

Chora mstari wa maisha ya Musa.
Swali: Tangu kuzaliwa kwa Yusufu hadi kuzaliwa kwa Musa ni miaka ngapi? Jibu: Hatuna muda halisi, lakini ilikuwa karibu miaka 380
Swali: Musa aliishi kwa miaka mingapi? Jibu: miaka 120.

## Mchezo wa 9

Amri 10



• Kwa shughuli hii, unahitaji mayai 10, vinguo vya kusafisha, na mtu mmoja wa kujitolea ambaye ako tayari kuchafuka.
• Kwa kila mojawapo ya amri 10, mtoto anashikilia yai.Tumia njia nyingi za kushikilia yai, kwa mfano: moja mkononi mwake, kwa mguu wake, kati ya magoti yake, chini ya mikono yake, kinywani chake, nk.
• Kila wakati utagundua kuwa inaendelea kuwa ngumu kushikilia yai lisianguka.Hatimaye, kwa amri ya 10, weka yai juu ya kichwa chake.
• Wakati wa mchezo, sema amri, na uwaeleze jinsi ilivyo rahisi kushikila yai moja, lakini inakuwa vigumu kufanya kazi ya kushikilia yote kumi.Kwa mfano, kwa amri ya 6, unasema vile ni rahisi kumwua mtu, kwa hiyo unaweka yai sehemu ambayo ni rahisi kushikilia (watoto wanaweza kukusaidia, kusema mahali pa kuweka yai). Lengo ni kuwaonyesha watoto kwamba sisi sote tumetenda dhambi, na tumeachilia yai kwa wakati mmoja au mwingine.


• Mwishoni, vunja yai lililo juu ya kichwa cha mtoto. (vunja yai na jiwe, watoto hawafai kuona jiwe.Usigonge kichwa cha mtoto kwa sababu ataumia). Hakikisha mtoto anajua kwamba atachafuka kutokana na hili. Hii ni somo la kushuhudia la nguvu sana.

Amri 10

1. Usiwe na miungu mingine
2. Usifanye sanamu yoyote au kuiinamia
3. Usiseme jina la Mungu bure
4. Hifadhi siku ya kupumzika
5. Waheshimu baba na mama yako
6. Usiue
7. Usizini
8. Usiibe
9. Usifanye ushuhuda wa uwongo (kusema uwongo ili kumweka mwingine kwenye shida)
10. Usitamani vya mwenzio

## Majibu ya 9 ya mafumbo

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | K | A | U | G | N | U | M | F | L | A | M |
| S | I | U | A | B | P | F | A | K | R | O | P |
| O | C | G | U | A | W | A | M | I | S | R | I |
| T | H | N | K | H | B | A | H | C | O | A | G |
| O | G | I | P | A | M | F | N | H | M | N | O |
| T | K | W | F | O | H | A | K | A | S | U | M |
| A | P | A | I | L | A | S | U | K | A | H | I |
| W | A | M | I | K | S | R | I | A | M | A | S |
| M | O | T | O | R | B | W | A | T | O | T | R |
| B | W | T | S | O | B | M | I | F | T | O | I |






## Maswali na majibu ya 9

1. Kama Mungu atanisamehe, mbona nisifanye dhambi? (Shida ya Warumi 7. Mbona tuwe waangalifu na kutofanya dhambi kama Mungu atatusamehe? Dhambi huenda kinyume na Mungu na ni lazima iadhibiwe. Yesu hutusamehe, lakini daima kunayo madhara ya dhambi. Kwa mfano, ikiwa nitakosa darasani, Mungu anaweza kunisamehe lakini nitaadhibiwa).
2. Nini kitafanyika ikiwa nitafanya jambo mbaya, mbaya sana? (Swali hili linapaswa kuwasaidia wanafunzi wagundue kwamba Mungu husamehe hata dhambi kubwa, lakini bado tunahitaji kutubu na kuomba msamaha.Pia, ikiwa tuaumiza mtu vibaya sana, tunaweza kufungwa jela ingawa Mungu ametusamehe. Pia eleza kuhusu madhara yanayotokana na utumiaji wa madawa ya kulevya, vita, au ngono ambazo zinaweza kubadilisha maisha yetu yote ya baadaye na kuadhiri ndoto zetu).
3. Je, ni sawa kama nilitaka kufanya kitu kizuri, lakini nikajipata nikifanya kitu kibaya? ( Huu ni mvutano kati ya nia zetu na matendo yetu.Mungu anajali nia zetu, lakini Paulo anauliza, "Je, Tutende maovu ili wema udhihirike? " Jibu ni, " Hapana!" - Warumi 3: 5-8).

## Mahudhurio ya 9




Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:
Musa

## Kazi ya nyumbani 9

### Kazi

Kazi yako ni kuandika kile huwa unafanya baada ya kutenda dhambi, kama vile kutoisema, kudanganya ili usijulikane na kufanya dhambi nyingine. Wakati mwingine tunajidharau na kusema, "Mimi si mtu mzuri sana, hivyo sipaswi kuruhusiwa kufanya kitu fulani," na tunakata tamaa. Lakini jambo sahihi ni kukubali tu kwamba tumefanya dhambi na kumwomba Yesu atusamehe dhambi hiyo. Mungu hataki ukate tamaa kwa sababu umetenda dhambi. Anataka kukusamehe, ili uwe huru na uweze kuhamasisha watu wengine ili watubu dhambi zao.

### Soma

Siku ya 1: Hesabu 13:1-3, 17-25
Siku ya 2: Hesabu 13:26-33
Siku ya 3: Hesabu 14:1-9
Siku ya 4: Hesabu 14:10-16
Siku ya 5: Hesabu 14:17-24

# 10. NDIO, UNAWEZA



**Shujaa: Kalebu**
**Hesabu 13:1-3, 13:17-14:9, 14:7-24, 14:30-45**

## Fungu la 10 la Kumbukumbu

"Lakini mtapokea nguvu akishawajilia Roho Mtakatifu, nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu na Yudea yote na Samaria, hadi mwisho wa dunia." Matendo 1:8

## Hadithi ya 10 ya Uhitaji



Katika shule ya Jumapili, Peppy alisoma kwamba Mungu anataka tushiriki imani yetu ili watoto wengine waweze kumwamini Yesu, pia.Siku ya Jumatatu, aliporudi shuleni kutoka likizo, Peppy aliona msichana aliyekuwa ameketi peke yake. Alipokuwa akirudi darasani, akamwambia rafiki yake Comet, "Je, umemwona msichana huyo kwenye kiti? Nadhani ana upweke sana." Comet akajibu, "Labda unaweza kwenda na kumchangamsha. Unaweza hata kumwambia kuhusu Yesu na kumwalika kanisani ili asijihisi mpweke tena." Peppy akasema, "Lakini nitasema nini? Sijui cha kumwambia. Na marafiki zangu watafikiria nini? "

## Somo Kuu la 10

Baada ya mamia ya miaka, Mungu alikuwa akiiongoza Israeli ili kutimiza ahadi Yake kwa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo. Mungu alimwambia Musa awatume wapelelezi 12 ili kuipeleleza nchi ya ahadi.Walirudi na kusema, 'nchi inatiririka maziwa na asali, na hili ni tunda lake ambalo ni kubwa sana. Lakini wenyeji wake ni wenye nguvu sana, na miji yao ni imara na mikubwa sana'. Lakini wapelelezi 10 walisema kuwa Waisraeli hawawezi kupigana na watu hao kwani wana nguvu nyingi. Mmoja wa wapelelezi, Kalebu, alipinga, akisema "Tunaweza kuwashinda." Aliamini kwamba Mungu wake mwenye nguvu angewasaidia. Mungu hupendezwa na imani ya aina hiyo.

Lakini watu waliwaamini wapelelezi hao wengine, wakajawa na hofu, wakakataa kwenda. Mungu aliwakasirikia sana, na adhabu kwa wale watu kumi ilikuwa kifo! Adhabu kwa taifa zima ilikuwa kutembea jangwani. Walipoasi, walishindwa kwa urahisi kwa sababu Mungu hakuwa pamoja nao. Baada ya kutembea kwa miaka 40, wale pekee waliosalia kutoka kwa kizazi hicho walikuwa Kalebu na mpelelezi mwingine aitwaye Yoshua ambaye alikubaliana naye. Kama malipo kwa imani yao, Mungu aliwapa nchi waliokuwa wamepeleleza.

Mapema leo tuliona kwamba Peppy aliogopa, lakini Comet alikuwa na ujasiri katika imani yake na kumsaidia Peppy. Mungu hupendezwa tunapozingatia imani yetu na kumtii katika kitu ambacho kinaonekana kama hakiwezekani. Mungu ana mpango juu ya maisha yako ambao ni zaidi ya unachoweza kudhania ikiwa tu utamkubali.

Yesu alisema kwamba ikiwa una imani kama mbegu ya haradali, unaweza kufanya milima kusonga (Mathayo 17:20). Tunaweza kukuza imani yetu kama mbegu kwa kufuata na kutumikia viongozi kutoka kanisa letu. Yoshua alikuwa msaidizi wa Musa (Kutoka 24:13). Musa angeingia katika hema kuongea na Mungu, lakini alipoondoka, Yoshua alibaki katika hema pamoja na Mungu (Kutoka 33:11). Tunaweza kutumia muda wetu pamoja na Mungu, pia, kwa kusoma Biblia, kuomba, na kuimba nyimbo Kwake na

sio tu tunapokuwa na watu wengine bali pia wakati tuko peke yetu. Tunaweza kukumbuka mambo ambayo Mungu amefanya katika Biblia na katika maisha yetu. Kalebu na Yoshua walishuhudia miujiza ambayo Mungu alifanya huko Misri. Tunaweza kuchagua marafiki ambao watatutia moyo, jinsi Yoshua alijiunga na Kalebu katika kuwatia moyo wengine. Kwa upande mwingine, Waiisraeli hao wengine walijiunga na wapelelezi ambao hawakuamini. Kama una rafiki ambaye imani yake inakuathiri visivyo, basi unaweza kumwacha na kutumia muda wako mwingi na marafiki wanaoamini. Imarisha imani yako ili wakati Mungu atakuita, unaweza kumtii na kuishi maisha mazuri ambayo amekuandalia, na pia uweze kuwatia moyo wengine kufanya hivyo.
Naamua kusema ndiyo kwa Mungu. Bwana, nakupa udhibiti wa maisha yangu kufanya mambo Unayotaka, yawe makubwa, madogo, au hata yawe hatari.Maisha yangu niYako .Nisaidie niishi kwa ajili yako bila hofu au kunung'unika.Tafadhali fungua macho yangu ili niweze kuona mipango mingi uliyo nayo juu yangu. Asante.

## Suluhisho la 10



Wakati wa chakula cha mchana Comet akasema, "Na, je, nikienda na wewe itakuwaje?Hebu tuende tuketi pamoja na msichana huyo. Hata mimi sijui cha kusema, labda Mungu atatusaidia sisi wote kuwa wazuri kwake." Peppy alifurahi kwamba Comet alikuwa rafiki yake na angemsaidia kushiriki imani yake na msichana yule. Msichana alikuwa na matatizo ya kinyumbani lakini kwa kufanya marafiki wapya na kujifunza kwamba Yesu anampenda ilimfanya ahisi vizuri sana.

## Shughuli ya 10

Barua kwa Mungu




Katika shughuli hii, kila mtoto katika darasa anaandika barua kwa Mungu akisema kile anataka Mungu afanye na maisha yake. Himiza watoto waandike mambo makuu—Mungu ni mkuu. Watoto wanapaswa waombe kuhusu hili wakienda nyumbani kwa wiki nzima na kuongeza mambo mapya wanayotaka.


## Mstari wa 10 wa wakati

Chora mstari wa maisha ya Kalebu.
Swali: Musa alikuwa na umri wa miaka mingapi wakati Kalebu alizaliwa? Jibu: Hatuna umri wake halisi, lakini inadhaniwa kwamba Musa alikuwa na umri wa miaka 40
Swali: Kalebu aliishi kwa miaka mingapi? Jibu: Hatuna muda halisi lakini inadhaniwa aliishi miaka 110.

## Majibu ya 10 ya Mafumbo

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| U | T | A | W | Y | O | S | H | U | A | Z | I |
| W | A | T | A | O | I | N | A | A | N | A | K |
| N | I | K | P | D | I | R | U | Z | I | K | A |
| A | S | A | E | A | H | A | D | I | W | I | L |
| A | S | N | L | K | Y | A | H | W | A | N | E |
| L | A | A | E | A | O | S | B | A | N | U | B |
| I | N | A | L | B | U | N | W | U | E | G | U |
| B | A | U | E | I | W | S | A | T | L | N | M |
| A | W | I | Z | A | M | A | N | A | E | U | A |
| K | A | B | I | H | D | R | A | I | L | N | Z |





## Maswali na majibu ya 10

1. Ni mambo gani magumu ambayo Mungu amekuomba ufanye? (Ongea na wanafunzi wako kuhusu hali tofauti katika maisha yao).
2. Itakuwaje nikijiumiza au nijiingize katika hali ngumu kwa sababu ya kufanya kile naamini Mungu aliniita kufanya? (Wengi wamepoteza maisha yao kwa kumtii Mungu, hivyo bila kujali ugumu, ni vizuri kumtii Mungu badala ya kumuasi.
3. Nitawezaje kuhakikisha kwamba sauti niliyosikia ni ya Mungu? (Unaweza kuangalia uamuzi wowote kupitia kanuni hizi 3 zinazopendekezwa: 1. Biblia: Je! Jambo hili linalingana na Biblia? 2. Mamlaka zangu: wazazi wangu, au mchungaji wangu ana maoni gani kulihusu? Roho yangu: Bibilia inasema kwamba sisi ni kondoo wa mchungaji mwema na tunaweza kutambua sauti yake.Lazima tujifunze jinsi ya kusikiliza

roho yetu kabla ya kufanya au kutofanya kitu.Kupitia kanuni hizi, ikiwa tunaamua kwamba ni sauti ya Mungu, tunapaswa kuitii, hata ikiwa ni jambo linaloonekana kama haliwezekani!)

## Mchezo wa 10

Nani Amepotea?



- Watoto wanaketi katika umbo la mduara na kufunga macho yao.
- Mwalimu anamgusa mtoto, ambaye anaenda na kujificha.
- Waulize watoto watambue ni nani amepotea.
- Chaguo: Unaweza kuweka vitu kadhaa katikati ya mduara wa watoto.Wakati watoto wanafunga macho, mwalimu anaondoa kitu kimoja na watoto wanapaswa kugundua kitu kilichoondolewa.

## Mahudhurio ya 10




Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa!
Kadi ya leo ni:
Vitabu vya Kihistoria

## Kazi ya nyumbani 10

### Kazi

Wiki hii kazi yako ni kuandika mambo matano mazuri ambayo Mungu amekufanyia. Kisha fikiria kuhusu mtu katika maisha yako ambaye anaweza kubaliana na wewe kuwa mambo hayo umesema ni mazuri. Watu kama hao ndio unaopaswa kutumia muda mwingi ukiwa nao. Fikiria kuhusu mambo unayostahili kubadilisha kila siku ili uweze kutumia muda mwingi na marafiki kama hao. Tayari una imani. Hii itasaidia imani yako kukua zaidi, kama kunyunyizia mmea maji na kuusaidia kukua.
Soma
Siku ya 1: Hesabu 22:1-8
Siku ya 2: Hesabu 22:9-17
Siku ya 3: Hesabu 22:18-25
Siku ya 4: Hesabu 22:26-33
Siku ya 5: Hesabu 22:34-41

# 11. USIDHUBUTU KUFANYA



**Hadithi ya Biblia: Balaamu**
**Hesabu 22:1-6, 22:9-38, 23:13-21, 24:10-13**

## Fungu la 11 la Kumbukumbu

"Watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, kwa maana kufanya hivyo ni vizuri."
Waefeso 6: 1

## Hadithi ya Uhitaji ya 11



Buzz alitaka kuhudhuria mkutano uliokuwa unafanyika katika mji wake.Aliharakisha kumaliza kazi yake ya nyumbani na kumsaidia mama yake kusafisha nyumba, ili apate ruhusa ya kwenda. Alimaliza na kumwambia mama yake, "Mama, unaweza kunipa ruhusa ya kwenda mkutano leo alasiri kati ukumbi mkuu?"Mama yake akamjibu, "Kwa leo haitawezekana. Tunataka kuondoka, na tunataka ukae hapa nyumba." Buzz akahuzunika na akachanganyikiwa. Mamake anawezaje kosa kumpa ruhusa ya kwenda? Wakati huo huo, Kip, mwenzake wa shule ya Jumapili, akamwita na kumwuliza, "Je! Unakuja? Tukusubiri, ama twende? " Buzz akasema, "Hapana, siendi." Kip alisema, "Buzz, hili ni jambo la Mungu. Unaweza kwenda. Mungu ni muhimu zaidi kuliko kila kitu! "

## Somo Kuu la 11

Wiki iliyopita, Waisraeli walianza kutembea jangwani kwa miaka 40. Walipokuwa wakisafiri, walivuka eneo la taifa la Moabu. Wamoabu waliogopa sana, na mfalme wa Moabu aitwaye Balaki akatumana ili mtu mmoja aitwaye Balaamu aje awalaani.Balaamu alimwuliza Mungu afanye nini, naye Mungu akamwambia asiende. Lakini mfalme Balaki akakasirika na kutaka Balaamu aje. Hivyo, mfalme alikawatuma maofisa wakuu na akaahidi kuwa atampa Balaamu zawadi kubwa.Balaamu akawaambia wasubiri uamuzi wa Mungu. Wakati mwingine tunakosa kukubaliana na Mungu, na tunataka kumwuliza tena ili kuhakikisha au tunataka abadilishe mawazo Yake. Mungu alimruhusu aende lakini alikasirika. Wakati mwingine tunapotaka Mungu abadilishe mawazo, Anaturuhusu tupate kile tunataka na pia madhara yake. Balaamu alipokuwa akienda Moabu, malaika akasimama barabarani mbele yake. Balaamu hakuona, lakini punda wake aliona. Kwanza punda wake aliondoka barabarani na kuingia shambani, kisha akaenda chini ya barabara na kujisukumiza ukutani na kuubana mguu wa Balaamu hapo, kisha baadaye akalala chini. Wakati huu Balaamu akawaka na hasira, Mungu naye akamruhusu punda kuzungumza! Akasema, "Mbona unanikasirikia? Je, si mimi ni yule yule punda wako? Je, nimewahi kukutendea namna hii?" Kisha Mungu akamruhusu Balaamu kumwona malaika ambaye angeweza kumwua, na Balaamu akagundua kile alichokifanya kilikuwa kibaya. Balaamu alitambua kwamba Mungu hakutaka alaani Israeli, bila kujali ukubwa wa zawadi ambayo angeweza kupata kutoka kwa mfalme Balaki .Walipofika, Balaamu alibariki Israeli mara nne na hakufikiria kamwe kuhusu kumuasi Mungu tena.
Mapema leo tulisoma jinsi Buzz anajaribiwa kuasi mzazi wake na kwenda mkutanoni. Ni rahisi kwake kuwa na sababu za kwenda, kama vile kutumia sababu ya Kip kwamba mkutano huo unahusu Mungu. Lakini Mungu ametuamuru tuwatii wazazi wetu, na amri ya Mungu haitabadilika kwa sababu ya

mkutano. Yesu alisema tukeshe tukiomba, ili tusije tukaingia katika majaribu. (Mathayo 26:41). Kuwa makini kile unawaza kwa sababu unapowaza kuhusu kufanya mambo mabaya wakati mwingi, inakuwa vigumu sana kufanya jambo linalostahili. Mara tu unakumbuka kile Neno la Mungu linasema, litii kwa haraka iwezekanavyo ili usiwe na nafasi ya kufanya makosa.
Naamua kumtii Mungu kwa haraka iwezekanavyo na sitajiruhusu kuwaza mabaya.

## Suluhisho la 11




Wakati huo huo, Buzz alikumbuka kwamba Neno linasema kwamba tunapaswa tutii wazazi wetu na kwamba Mungu anapendezwa nasi tukiwa watiifu. Kisha akasema, "Mimi siendi." Aliambia Kip kile Neno linasema tunapaswa kufanya.

## Shughuli ya 11

Pete za Kamba za Mpira
Wakati wa darasa, watoto wanaunda pete ya kidole au bangili kwa kutumia kamba ya mpira ili kuwakumbusha wiki yote kwamba hawapaswi kushinikiza Mungu abadilishe mawazo yake.Fuata michoro kwa maelekezo ya kuunda au unaweza kutumia pete za plastiki.

1. Chukua kamba ya mpira na uikunje nusu.
2. Ingiza mpira mwingine kupitia vifungo vya mpira wa kwanza.
3. Kunja mpira katika nusu ili kuunda bangili. Rudia hatua hizi hadi uunde bangili ya ukubwa unaotaka.
4. Tumia mpira mwingine ili kufunga pamoja pande za mwisho.




## Mstari wa 11 wa wakati

Andika wakati ambapo hadithi ya punda wa Balaamu ilitokea.
Swali: Musa alikuwa na umri wa miaka mingapi wakati watu wa Mungu walianza kutembea jangwani?
Jibu: umri wa miaka 80
Swali: Balaamu alianza lini kufanya kazi dhidi ya watu wa Mungu? Jibu: Wakati walipokuwa wakitembea jangwani.

## Majibu ya 11 ya Mafumbo

Vitabu vya Biblia
Andika vitabu vya Biblia kwa utaratibu kutoka Mwanzo hadi Esta.
1.Mwanzo
2. Kutoka
3. Leviticus
4. Hesabu
5. Kumbukumbu la Sheria
6. Yoshua
7. Waamuzi
8. Ruthu
9. 1 Samweli

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Y | E | N | Y | E | N | G | U | V | U | B | I |
| K | U | S | I | S | I | T | I | Z | A | M | A |
| K | S | I | T | I | Z | A | K | L | W | A | N |
| W | I | K | I | L | A | B | A | U | S | L | A |
| A | W | I | K | I | R | A | B | E | M | A | W |
| T | A | L | A | A | M | A | P | U | Z | I | B |
| U | L | O | S | U | D | A | W | G | O | K | W |
| W | A | A | D | N | U | P | A | N | G | A | E |
| P | A | W | E | L | O | K | O | U | K | B | N |
| I | N | G | U | V | D | H | A | M | B | I | A |
| G | I | B | M | A | K | A | G | I | P | U | K |

10. 2 Samweli
11. 1 Wafalme
12. 2 Wafalme
13. 1 Mambo ya Nyakati
14. 1 Mambo ya Nyakati
15. Ezra
16. Nehemiya
17. Esta



## Maswali na majibu ya 11

1. Napaswa kufuata ushauri wa nani? (Kwanza, Mungu, kisha mamlaka iliyo juu yako hapa duniani. Kumbuka, hata hivyo, kwamba tunaweza kuwa na hakika kwamba tunamfuata Mungu ikiwa mamlaka juu yetu inakubaliana na kile tunadhani tunahisi).
2. Je, itakuwaje wazazi wangu wakiniamrisha kufanya kitu kibaya? (Ongea kuhusu hali tofauti ambazo wazazi wanaweza kukosea. Wasaidie wanafunzi wako kuona jinsi wazazi huwaza, kwa sababu mara nyingi, wazazi huwa sahihi).
3. Je! Nitakuwa kiongozi lini? (Katika uzoefu wangu, hata wakati mtu anakuwa mzima, bado kuna hali ambazo Mungu atamwuliza atumikie wengine. Kwa wanafunzi ambao ni viongozi wenye vipaji, wahimize wasubiri mpaka wakati Mungu atawapa huduma yao. Kwa mfano, Yesu, aliwauliza viongozi wa kidini maswali magumu akiwa na umri wa miaka kumi na mbili, lakini Mungu hakumruhusu aanze huduma yake mpaka alipokuwa na miaka thelathini).

## Mchezo wa 11

Usidunge punda



- Chukua kadi na uchore punda katikati , na uache nafasi tupu kwa ajili ya upanga. Pia chora upanga wa ukubwa sawa na nafasi tupu.
- Fanya timu mbili au tatu za watoto na uchague mtoto kutoka kila timu.
- Patia mtoto uliyechagua upanga na wana timu wake wafunge macho.
- Timu itaelekeza mtoto wakisema aidha (kulia, kushoto, juu, chini). Wanajaribu kuelekeza upanga kwenye nafasi tupu ya kadi bila kumgusa punda.
- Kila timu inashindana, na kupata timu ya washindi.

## Mahudhurio ya 11

Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:




Upanga wa Bwana

## Kazi ya 11 ya nyumbani

### Kazi

Kazi yako wiki hii ni kuandika kuhusu kitu ambacho unapinga, jambo ambalo hutaki kufanya lakini unapaswa kufanya, au kitu unachotaka kufanya lakini hupaswi kufanya. Inaweza kuwa kitu rahisi kama kazi hii ya nyumbani au inaweza kuwa kitu ambacho wazazi wako wanataka ufanye. Fikiria kuhusu madhara yanayosababishwa na jambo hili katika moyo wako, kwa rafiki yako na familia yako, au matumaini na ndoto zako ya baadaye za kumtumikia Mungu. Kisha mwombe Yesu akusamehe na kulitakasa kutoka moyoni mwako, ukimwambia Yesu kuwa ndiye mfalme wako. Fuatilia ikiwa uasi uliondoka au la na kurudia sala hiyo jinsi unavyohitaji.

### Soma

Siku ya 1: Yoshua 5:13-6: 5
Siku ya 2: Yoshua 6:6-11
Siku ya 3: Yoshua 6:12-19
Siku ya 4: Yoshua 6:20-23
Siku ya 5: Yoshua 6:24-27

# 12. UPANDE WA MUNGU



**Shujaa: Yoshua**
**Yoshua 1:1-11, 2:1-21, 3:14-4:7, 4:15-18, 5:10-6:11, 6:15, 6:20-25, Waebrania 11:30-31**

## Fungu la 12 la Kumbukumbu

"Bali wote waliompokea na kumwamini aliwapa haki ya kufanywa watoto wa Mungu." Yohana 1:12

## Hadithi ya 12 ya Uhitaji



Kip ako karibu kumaliza mwaka wa shule . Ni wakati wa mitihani ya mwisho, na anajua lazima afanye vizuri ili aendelee kupata udhamini.Kesho ana mtihani wa kwanza, lakini leo, amekuwa akicheza na marafiki zake na akitizama katuni.Mwishoni mwa siku, anapoenda kulala, anaomba , "Mungu, tafadhali, nakuomba unisaidie kesho katika mtihani wangu. Lazima nifanye vizuri sana ili niendelee kupokea udhamini. Asante kwa kunisikia. Najua kwamba Wewe utanisaidia."

## Somo Kuu la 12

Unakumbuka jinsi Yoshua alijenga imani yake? Mungu alimchagua Yoshua kuongoza taifa na kumwahidi kwamba atakuwa pamoja naye daima.Baada ya kutembea kwa miaka 40 jangwani, ilikuwa wakati wa kuchukua nchi ya ahadi.Yoshua aliwatuma wapelelezi wawili kwenda mji wa Yeriko. Kahaba aitwaye Rahabu aliwaficha wapelelezi na kuwasaidia kutoroka kupitia dirisha ya nyumba yake, sehemu ya ukuta wa jiji.Nao wapelelezi wakamwahidi kuwa watamwokoa pamoja na familia yake ikiwa atafunga kamba nyekundu kwenye dirisha.

Kuvuka mto wa Yordani, makuhani walibeba sanduku la agano, ishara ya mahali ambapo Mungu alikuwa, na kutembea moja kwa moja kuelekea mtoni. Mto uliokuwa unafurika ukaanza kurudi nyuma kimiujiza.Hebu fikiria ukijaribu kuzuia maji mengi kwa mikono yako. Israeli walitembea juu ya ardhi kavu na kuchukua mawe 12 kutoka kwenye mto ili kuwa kumbusho ya kile Mungu alifanya.Tunaweza kuandika kuhusu kile Mungu anafanya katika maisha yetu, pia.Kisha Israeli waliadhimisha sikukuu ya Pasaka: unakumbuka wakati waliweka damu ya kondoo kwenye milango ya nyumba zao huko Misri ili kuokolewa?

Siku moja Yoshua alikutana mtu aliyekuwa na upanga.Akamwuliza kama alikuwa upande wa Israeli au upande wa adui. Mtu huyo alisema kuwa hakuwa upande wowote, bali alikuwa jemadari wa jeshi la Bwana. Mtu huyo alikuwa Yesu!

Wakati mwingine tunadhani kuwa Mungu yuko upande wetu tu kwa sababu tunajiita Mkristo au tunaenda kanisani.Wakati mwingine tunakosea, kama vile kukosa kusomea mtihani au hata kufanya dhambi, kisha tunamwomba Mungu kwa chochote tunachotaka na kujiuliza kwa nini Yeye hajibu.Ni sisi tunaopaswa kujiunga na upande wa Mungu , sio Mungu kujiunga nasi.Waisraeli walijiunga na Mungu katika sherehe ya Pasaka, ishara ya kumwamini Yesu.Rahabu alijiunga na Mungu kwa kuwasaidia watu wa Mungu na kufunga kamba nyekundu kwenye dirisha lake, ishara nyingine ya kumwamini Yesu.Wafarisayo, viongozi wa kidini wa Israeli wakati wa Yesu, walidhani walikuwa upande wa Mungu

lakini walikasirisha Mungu kwa kukosa kumwamini Yesu na kuwapotosha watu. Yesu akawaambia kuwa watoza ushuru na makahaba wangeingia ndani ufalme wa Mungu mbele yao kwa sababu waliamini na kutubu (Mathayo 21: 31-32). Hatuwezi kuweka imani yetu katika imani ya wazazi wetu au kwa sababu tunaenda kanisani, na hatupaswi kuwahukumu wengine kwa sababu ya mahali wanatoka.Haijalishi unatoka wapi, unapaswa kumwamini Yesu ili kuokolewa.
Waisraeli walizunguka jiji na kupiga kelele .Kuta zilianguka isipokuwa nyumba ya Rahabu, na Waisraeli wakateketeza mji huo.Rahabu hakujiunga tu na watu wa Mungu, lakini baadaye akawa nyanya wa nyanya wa mfalme Daudi na baadaye nyanya wa nyanya wengi wa Yesu (Mathayo 1: 5-6, 16). Naye Yoshua aliongoza taifa katika maisha yake yote.
Nimetambua kwamba kuwa miongoni mwa Wakristo haimaanishi kwamba Mungu yuko upande wangu .Naamua kujiunga na upande wa Mungu kwa kumwamini Yesu na Kumtii.


## Suluhisho la 12



Mtihani wa Kip ulikuwa mgumu sana, na angeweza kupita tu kama angesoma kwa bidii. Alimaliza mtihani na kutumaini kuwa kwa namna fulani Mungu atamsaidia. Baadaye matokeo yalitoka na Kip akaanguka mtihani kwa kuwa hakuwa amejitayarisha vilivyo. Kip akapoteza udhamini wake. Alihuzunika sana na akachukua simu yake na kumpigia rafiki yake Taffy ili amtie moyo katika hali hii ngumu.

## Shughuli ya 12

Kuta za Yeriko




Waache watoto waombe na kutafakari kwa dakika chache kuhusu kitu ambacho huwa kinawatenganisha na Mungu.Patia kila mtoto kipande cha karatasi kama ishara ya tofali moja ya kuta za Yeriko. Waambie waandike kwenye tofali la karatasi kitu chochote ambacho huwazuia au huwatenganisha na Mungu. Baada ya hayo, waambie wakunje karatasi ile na kwenda nayo nyumbani. Wahimize wawe wakiangalia karatasi wiki hii na waombe Mungu awaondolee ukuta huo unaowatenganisha Naye.


## Mstari wa 12 wa wakati

Chora mstari wa maisha ya Yoshua.
Swali: Musa alikuwa na umri wa miaka mingapi wakati Yoshua alizaliwa? Jibu: Hatuna umri wake halisi, lakini inadhaniwa kwamba Musa alikuwa na umri wa miaka 40
Swali: Yoshua aliishi kwa miaka mingapi? Jibu: miaka 110.

## majibu ya 12 ya mafumbo




| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| F | A | M | L | Y | U | B | A | H | A | R | O |
| M | A | W | E | L | O | K | O | U | K | K | A |
| U | K | N | V | M | A | A | D | U | I | V | U |
| N | U | G | I | K | U | T | A | R | A | K | H |
| G | G | U | T | K | Y | P | E | W | L | U | S |
| U | N | M | A | V | I | Y | A | A | A | A | O |
| B | A | R | A | K | A | W | L | N | M | N | Y |
| Y | U | A | I | L | I | M | A | F | D | G | U |
| F | K | V | H | A | B | U | W | A | Y | E | C |




## Maswali na majibu 12

1. Uliomba Mungu lini ili akusaidie katika kitu ambacho sio mapenzi yake? (Ongea kuhusu maombi ya kuchekesha kama vile kumwombea mtu kwenye televisheni, kuomba ili usipewe kazi, kuomba ili mwanafunzi mwingine apoteze mchezo, nk).
2. Mungu ni mkubwa sana; anawezaje kuwa rafiki yangu? (Ongea kuhusu mambo tofauti ya Mungu, kama ukuu wake, lakini pia upendo wake. Pia jadili ukweli kwamba anatujua nje na ndani).

3. Mungu anataka nini kutoka kwangu? (Sote tuna vipaji tofauti kutoka kwa Mungu na uwezo tofauti wa kimwili. Mungu anaweza kututumia sote kwa njia moja au nyingine ili kuonyesha utukufu wake katika ulimwengu huu na kuwafikia watu zaidi kwa ajili yake. Una vipaji vigani? Uwe na uwezo upi? Kumbuka pia, Mungu anaweza kututumia katika mambo ambayo hayalingani na vipaji na uwezo wetu. Wakati mwingine anataka kuonyesha ukuu wake kupitia udhaifu wetu. Anajali zaidi kuhusu moyo ulio tayari na unaoweza kufanya chochote anachotaka kutoka kwetu).

## Mchezo wa 12

Chora hili



- Weka bango lililo na fungu la kumbukumbu. Usiandike maneno kadhaa, uache nafasi wazi badala yake.
- Ili kucheza, wanafunzi wanatafuta fungu hilo katika Biblia, na kusema maneno gani yanayokosa kwenye bango.
- Katika nafasi tupu, wanafunzi wanachora picha ili kuwakilisha maneno yanayokosa. (Maneno yanayokosa yanaweza kuwakilishwa kwa mchoro zaidi ya mmoja).
- Ikiwa una watoto wengi, wagawanye katika timu 4 hadi 6 na ufanye nakala ya bango kwa kila timu.
- Baada ya kuchora picha, waambie wakariri mara kadhaa mpaka waweze kuelewa vizuri.

## Mahudhurio ya 12




Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:
Yoshua

## Kazi ya nyumbani 12

### Kazi

Kazi yako wiki hii ni kugundua ikiwa unajifanya kuwa Mkristo ili uwe na marafiki au ikiwa unamwamini Yesu. Ikiwa hii ndio mara yako ya kwanza au ikiwa hujui, mwulize mwalimu wako wa shule ya Jumapili jinsi unaweza kujiunga na familia ya Mungu kwa kumwamini Yesu. Ikiwa tayari umemkubali Yesu, basi sema kitu kizuri wiki hii kwa mtu ambaye si rafiki yako, kama kupongeza mavazi yake au jinsi anavyocheza michezo vizuri.

### Soma

Siku ya 1: Yoshua 7:1-12
Siku ya 2: Yoshua 7:13-19
Siku ya 3: Yoshua 7:20-26
Siku ya 4: Yoshua 8:1-13
Siku ya 5: Yoshua 8:14-29

# 13. USIBAKISHE CHOCHOTE



**Hadithi ya Biblia: Akani**
**Yoshua 6:17-19, 7:1-12, 7:20-8:7, 8:18-27**

## Fungu la 13 la Kumbukumbu

"Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwa minifu na wa haki na atatusamehe dhambi zetu na kututakasa na uovu wote." 1 Yohana 1: 9

## Hadithi ya 13 ya Uhitaji

Comet alikuwa darasani akimalizia kazi yake ya sayansi kabla ya kuisalimisha kwa mwalimu. Alitaka kupata alama za juu. Wakati huo huo rafiki yake akaingia, akikimbia karibu kuanguka, na akaangusha chini kazi ya Comet.Wakati ilianguka sakafuni, kazi ile iliharibika na Comet hakuwa na chochote cha kumpa mwalimu. Comet alikasirika sana, lakini kijana huyo aliomba msamaha mbele ya wanafunzi wote na mwalimu. Hivyo Comet hangeweza kufanya chochote. Hakuwa na chaguo bali kusema, "Umeomba msamaha, kwa hivyo nakusamehe."Lakini Comet kwa kweli hakumsamehe .Aliwaza, "Moja ya siku hizi nitamfanyia vivyo hivyo, pia yeye atajua vile mtu huhisi akipoteza kitu muhimu sana."Baada ya hapo, Comet alisubiri mwalimu kutoa kazi kubwa na muhimu. Siku moja mwalimu akapeana kazi kama hio.Comet alisema, "Hii ndiyo fursa yangu!" Wakati alipata nafasi nzuri, Comet alienda dukani ili kununua soda . Nia yake ilikuwa kumwaga ile soda "kiajali" kwenye kazi ya mwenzake.

## Somo Kuu la 13

Wiki iliyopita, Yoshua na Waisraeli walinyakua Yeriko.Mungu alikwa amewaambia kuwa kila kitu katika jiji la kwanza kilikuwa chake, na hivyo walipaswa kuchoma na kutojiwekea chochote.Vitu kutoka miji iliyobaki vingekuwa vyao.Katika maisha yetu, kitu cha kwanza kupata kwa kila jambo ni cha Mungu, tunapaswa kumpa Mungu.

Yoshua na Waisraeli walidhani kuwa itakuwa rahisi kunyakua mji wa pili wa Ai .Ulikuwa mji mdogo ukilinganishwa na miji ambayo Waisraeli walikuwa wameshinda tayari.Mungu hutupatia Roho Mtakatifu ili atusaidia kushinda dhambi na kufanya mambo mema kwa Mungu, kama kuwa wema kwa wazazi wetu. Kwa msaada wa Mungu, inaweza kuonekana kuwa rahisi zaidi. Waisraeli walituma watu wachache tu kupigana na jiji hilo, lakini wakati huu walishindwa kwa urahisi! Yoshua akamlilia Mungu, "Kwa nini umetuacha? Watu katika nchi hii watatuua wote, na hakuna mtu atakayeamini kuwa Wewe ni Mungu mkuu! "Mungu alimwambia Yoshua asimame na aache kupiga kelele, na kwamba kuna mtu aliyekuwa amechukua na kuficha vitu kutoka Yeriko na hio ndio ilikuwa sababu ya kupoteza vita, na hio ilikuwa kuasi na kumdanganya Mungu. Tuseme siku moja unawandanganya wazazi wako.Unaweza kuficha kitu kutoka kwa wazazi wako, walimu, na marafiki, lakini Mungu huona na anajua kila kitu .Siku chache baadaye utagundua ni vigumu sana kuwa mwema kwa wazazi wako, na utamlilia Mungu, na kumwuliza kwa nini Amekuacha.Badala yake, fanya kile Yoshua alifanya na kumwomba Mungu ikiwa umefanya makosa.Unapofanya hivi , Mungu atakusaidia kwa haraka kwa sababu anakupenda na anakutakia mema.Kama vile Mungu alivyojali kuhusu kile Israeli ilifanya kuliko kile ambacho nchi za jirani zilidhania, pia anajali zaidi kuhusu moyo wako. Biblia inasema kwamba ikiwa tutatukiri dhambi zetu, Mungu ni mwaminifu na mwenye haki na atatusamehe na atutakase kutoka kwa dhambi zetu. Wakati Mungu atakuonyesha mahali umekosea, nenda na urekebishe haraka. Ikiwa uliwadanganya wazazi wako, nenda

na uwaambie ukweli. Ikiwa uliiba kitu, rudisha mara moja. Ikiwa ulimdharau mtu, omba msamaha. Ikiwa unashikilia chuki kama Comet, msamehe mtu huyo na usilipize kisasi. Ikiwa umechukua kitu kutoka kwa Mungu, mrudishie. Ukitubu haraka, ndivyo Mungu atakusaidia haraka na uendelea na kushinda.
Mungu alionyesha Israeli kwamba mtu mmoja aitwaye Akani ndiye aliyekuwa amefanya dhambi .Waligundua kuwa alikuwa amechukua vazi, sarafu za fedha, na kipande cha dhahabu kutoka Jeriko na kuvizika katika hema yake.Walimchukua pamoja na vitu vyake na kuwaangamiza.Kisha, waliporudi kupigana na Ai, Mungu aliwasaidia kupata ushindi.
Nimeamua kutobakisha au kuficha kitu chochote kutoka kwa Mungu na kutubu wakati nimefanya makosa.

## Suluhisho la 13



Lakini alipokuwa akitafuta fursa hii, Taffy aligundua kile Comet alikuwa anataka kufanya. Kisha Taffy akamwambia kuwa kuweka chuki moyoni mwake na kukosa kusamehe haikuwa jambo nzuri. Mungu hapendi jambo hilo. Comet alielewa kwamba alikuwa karibu kufanya makosa. Walimwomba Mungu na alimsamehe mwenzake.

## Shughuli ya 13

Sio yangu



Ambia watoto waweke vitu vya kibinafsi katikati ya meza. Chukua mojawapo ya vitu na kumwuliza mtoto mmoja, "Je, hii ni yako?" Ikiwa siyo yake, mtoto anapaswa kujibu, "Sio yangu na sitatamani au kuchukua kitu ambacho si changu." Rudia hii kwa kila kitu kilichowekwa, ili kila mtu ashiriki. Ikiwa watoto ni wachanga, rahisisha jibu na kuwa, "Sio yangu."

## Mstari wa 13 wa wakati

Andika wakati ambapo hadithi ya kutotii kwa Akani ilitokea.
Swali: Yoshua alikuwa na umri wa miaka mingapi wakati walishinda Ai? Jibu: Hatuna umri wake halisi, lakini inadhaniwa kwamba Yoshua alikuwa na umri wa miaka 70.
Swali: Ni wakati upi Akani alimuasi Mungu? Jibu: Wakati Yoshua na Waisraeli walipigana na Jeriko.

# Majibu ya mafumbo 13

Kila alama ni mara ngapi?

| 1 | 5 | 7 | 0 | 8 |
|---|---|---|---|---|
| 40 | 25 | 10 | 52 | 27 |

| 4 | 6 | 2 | 9 | . |
|---|---|---|---|---|
| 19 | 21 | 17 | 30 | 39 |

| | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 5 | 0 | 4 | 9 | 0 | 8 | 0 | . | 2 | 1 | 4 | 8 | 0 |
| 0 | 1 | 5 | 6 | 1 | 6 | 9 | 4 | 1 | 0 | . | 0 | 6 | 1 |
| 6 | 9 | 1 | 0 | 9 | 7 | 1 | 0 | . | 5 | 8 | 1 | 5 | 8 |
| 0 | 6 | 9 | 2 | 5 | 0 | 8 | 5 | 0 | 6 | 0 | 7 | 4 | 2 |
| 7 | 1 | 0 | 6 | 1 | . | 9 | . | 2 | 1 | 9 | 0 | 9 | 1 |
| 8 | . | 4 | 0 | 8 | 0 | 1 | 5 | 0 | 4 | 8 | 1 | 5 | 6 |
| 4 | 0 | 9 | 7 | . | 4 | . | 9 | 8 | 5 | 6 | 2 | 5 | 0 |
| 1 | 2 | 1 | 4 | 1 | 5 | 0 | 1 | 5 | 6 | 1 | 0 | . | 8 |
| 4 | 8 | 4 | 8 | 6 | 0 | 2 | 5 | 9 | 1 | 9 | 2 | 5 | 1 |
| 8 | 5 | 0 | 9 | 8 | 1 | 8 | 7 | 0 | . | 8 | 1 | 6 | 8 |
| 1 | 9 | 1 | 0 | . | 4 | . | 2 | . | 5 | 9 | . | 0 | 9 |
| 6 | 0 | . | 4 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | . | 1 | 0 | . | 0 |
| 0 | 8 | 5 | 6 | 0 | 8 | 5 | . | 0 | 9 | 0 | . | 5 | 6 |
| 1 | . | 1 | 0 | 1 | . | 6 | 1 | . | 5 | 1 | 2 | 4 | 8 |
| 9 | 6 | 9 | . | 9 | 7 | 8 | 0 | . | 4 | . | 0 | 9 | . |
| 2 | 0 | 8 | 0 | . | 4 | 9 | 8 | 2 | 8 | 0 | . | 6 | 0 |
| 7 | 2 | 1 | . | 5 | 0 | 1 | . | 7 | 9 | 1 | 9 | 7 | . |
| . | 4 | . | 0 | 2 | 4 | 6 | 0 | . | 4 | 6 | 2 | 0 | 8 |
| 9 | 5 | 9 | 9 | 0 | . | 7 | 9 | 1 | . | 0 | 5 | . | 9 |
| 0 | 2 | 8 | 5 | 9 | 5 | . | 8 | 6 | 0 | 2 | . | 0 | 1 |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | F | A | M | I | D | S | H | E | V | D |
| W | N | F | U | R | A | H | I | N | I | H |
| B | W | A | N | A | I | I | A | Z | T | U |
| H | C | M | G | W | H | N | W | M | A | S |
| A | H | I | U | A | F | D | A | B | B | H |
| S | O | L | S | Z | U | W | E | K | A | I |
| K | U | I | B | A | R | A | S | H | A | N |
| Z | R | A | W | Z | O | K | O | H | C | D |
| A | I | L | B | I | B | I | B | L | A | I |




# Maswali na majibu ya 13

1. Ni mambo gani ulificha ambayo Mungu anajua kuhusu? (Kuwa na muda wa kuzungumza na kuwakumbusha kwamba ikiwa mtu atashiriki jambo kwa ujasiri basi hapaswi kurirudia).
2. Je, kuna nafasi ya pili kwa Mungu? (Bila shaka, lakini pia fikiria jinsi tunavyojaribu kuwashawishi wazazi wetu watupatie fursa ya pili, lakini tunataka kuendelea kufanya jambo lile lile).
3. Je ni sawa kusema, Ni maisha yangu, muda wangu na fedha zangu? (Unapokuwa Mkristo wa kweli, na unakabidhi yote kwa Bwana, utagundua kuwa vitu unavyodhani ni vyako si vyako).

WOW! YEAH!!


## Mchezo wa 13

Kadi ya Muziki



- Toa kadi kwa kila mwanafunzi iliyo na neno la kumbukumbu. Kisha watoto waketi katika umbo la mduara.Hakikisha maneno hayapo katika utaratibu sahihi.
- Wakati muziki unaanza kucheza, watoto wanapitisha kadi zao kuzunguka mduara.
- Wakati muziki unasimama, wanafunzi wanasoma kadi walizoshika kulingana na utaratibu wa kumbukumbu.
- Baada ya kucheza zamu kadhaa, watoto wanaenda mbele na kadi zao na kuzipanga kwa utaratibu wa kumbukumbu.
- Rudia kumbukumbu mara kadhaa pamoja.

## Mahudhurio ya 13




Toa kadi ya leo kwa watoto waliohudhuria darasa. Washukuru na uwahimize wafike tena wiki ijayo ili kupata kadi nyingine ili waweze kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:

Dhahabu iliyofichwa

## Kazi ya nyumbani 13

### Kazi

Kazi yako wiki hii ni kuandika kuhusu kitu unachoficha kutoka kwa Mungu na kutoka kwa wengine na sababu ya kuficha. Kisha fikiria jinsi kufanya hivi kunakuathiri. Inadhuru ushirika wako na Mungu, na hilo si nzuri. Lakini, kama vile kulifanyika huko Ai, hili linaumiza darasa lako na watu ambao pamoja mnamfuata Yesu. Kwa sababu fulani huenda wasiweze kugundua. Lakini wewe unajua unachostahili kufanya. Tubu dhambi kwa Yesu na kwa wazazi wako au mwalimu unayemwamini au mchungaji. Mwombe Mungu msamaha na usubiri mabadiliko yanayosababishwa na msamaha wake.

### Soma

Hakuna kazi ya nyumbani wiki hii.